Nipashe
Jumatano Februari 3, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580480
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

**MAPATELI**, watukanaji mtandaoni dawa yao sasa yapatikana

UKURASA 3



**ADAIWA** kukamatwa na kiwanda, mitambo ya kutengenezea silaha

UKURASA 5


siasa
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje China ilivyozaa matunda
UCHAMBUZI
TEHAMA MPYA, UTAWALA BORA WA UTUMISHI UMMA
- Uzembe wa watawala 'stop'
- Mishahara bayana kila kona
- Mabilioni serikali yaokolewa
- Nusura ada mwaka Sh. mil. 302
- Ubunifu wa wataalamu wazawa

UKURASA 11

# Mbunge azua jambo mikopo elimu ya juu

**ASEMA** makato asilimia 15 yanawaumiza wanufaika, ataka serikali kufanya marekebisho...*Endelea Uk. 2*



Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, akizungumza katika mkutano wa pili, kikao cha kwanza cha Bunge la 12, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**



## Tume ya RC yabaini kifo dereva wa lori

UKURASA 3

UKURASA WA 8

## WADAIWA SUGU NHC KIKAANGONI

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) linatarajia kuanza uchambuzi kwa wadaiwa sugu wa nyumba zake katika mikoa 24 ya Tanzania Bara, ili kuchukua hatua za kisheria dhidi yao.

Uamuzi huo unatokana na wadaiwa muda waliopewa kukamilisha malipo ya malimbikizo kumalizika Januari 31, mwaka huu.

Meneja Uhusiano na Huduma za Jamii wa (NHC), Muungano...

## Shule yadaiwa kugeuzwa makazi ya nyani, ngedere

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAJIPANGA KUFANYA MAKUBWA UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK. 6

# Mbunge azua jambo mikopo elimu ya juu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, ameitaka serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kwa kuwa makato ya asilimia 15 ya mkopo yanawaumiza wanufaika.

Novemba, 2016, Bunge lilipitisha muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Namba nane ya mwaka 2016 pamoja na mambo mengine, ukipendekeza kurekebisha Sheria ya Bodi hiyo ili mnufaika wa mkopo arejeshe mkopo kwa makato si chini ya asilimia 15 ya mshahara wake kila mwezi badala ya asilimia nane iliyokuwapo awali.

Akiuliza jana swali la nyongeza bungeni, mbunge huyo alisema makato hayo ni makubwa na kuwaumiza wanufaika ambao wengi wao ni watoto wa maskini.

"Watanzania wengi ambao wamemaliza kidato cha sita wanatamani kupata mikopo ya elimu ya juu ili kuwa na wataalamu wa fani mbalimbali, lakini mikopo hii inayotolewa tumeweka makato makubwa ya asilimia 15 na penati ya asilimia sita. Tunakuta wanufaika wengi ambao ni watoto wa maskini, wanashindwa kuhimili," alisema.

Alihoji: "Ni lini sasa serikali italeta marekebisho ya sheria hii, ili tupeleke kwenye tarakimu moja yaani asilimia nane hadi tano ili tutoe wajuzi badala ya kugeuzwa kama chanzo cha mapato?"

Akijibu swali hilo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema lengo la serikali ni mikopo hiyo ijiendeshe kwa wanufaika kurejesha mikopo na makusanyo yatosheleze kutoa mikopo kwa wanafunzi wengine.

"Hadi sasa makusanyo ya mikopo yanachangia mikopo kwa asilimia 46 ya bajeti ya mikopo, asilimia 15 anayokatwa anabaki na asilimia 85 na tukumbuke mkopo wa Bodi ndio uliotangulia mikopo mingine na kwa taratibu za kiutumishi mtumishi anapaswa abaki na theluthi moja ya mshahara baada ya makato," alisema.

Aidha, aliwasihi wanaochukua mikopo kutambua umuhimu wa kulipa na kama wana fedha wasisubiri kukatwa hizo asilimia 15.

"Watambue umuhimu wa kurejesha mikopo kwa kuwa mikopo hiyo inasaidia wengine wanufaike na mikopo hiyo," alisema.



Baadhi ya wabunge wakiingia katika viwanja vya Bunge tayari kwa kuhudhuria Bunge la 12, mkutano wa pili, kikao cha kwanza, jijini Dodoma jana.. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Shule yadaiwa kugeuzwa makazi ya nyani, ngedere

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Ulyankulu (CCM), Rehema Migila, ameiomba serikali kuifungua Shule ya Sekondari Isike iliyoko mkoani Tabora ambayo imegeuka kuwa makazi ya ngedere na nyani.

Shule hiyo ilijengwa kwa ajili ya kuhudumia wakimbizi na jamii inayowazunguka, lakini baada ya wakimbizi kurudi kwao na kubaki na wanafunzi wachache, serikali iliwahamisha wanafunzi waliobaki na kuwapeleka Shule ya Sekondari Ulyankulu.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema shule imefungwa haifanyi kazi yoyote na imekuwa ni makazi ya ngedere na nyani hali inayosababisha wananchi na serikali kuonekana wametupa nguvu bure.

Alisema Shule ya Sekondari ya Ulyankulu imezidiwa wanafunzi na kulazimika wengine kuhamishiwa shule ya Mkindo ambayo si ya bweni.

"Je, serikali haioni sasa kuna haja ya kuwarudisha wanafunzi ambao wanatembea umbali mrefu na kuwaongezea wazazi gharama ambazo hazihitajiki? Shule imefungwa haifanyi kazi yoyote imekuwa ni makazi ya ngedere na nyani hali inayosababisha wananchi na serikali kuonekana wametupa nguvu bure," alihoji.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itaifungua shule hiyo.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema shule hiyo ilijengwa kwa ajili ya kuhudumia wakimbizi na kwamba kufungwa kwake kulizingatia matumizi sahihi ya rasilimali watu, fedha na vifaa.

Hata hivyo, alisema serikali itafungua shule hiyo endapo itabainika kuna mahitaji.

Akiongezea majibu ya maswali hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Selemani Jafo, alimwagiza Ofisa Elimu wa Mkoa wa Tabora kufanya tathmini ya haraka na kutoa majibu ili kuwasaidia watoto wa eneo hilo.

# Ndugai aipa mtihani Kamati ya Huduma

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameipa mtihani mzito Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, akiitaka kwenda kasi kwenye suala la bima ya afya kwa wote, kwa kuwa wasipojipanga vizuri ndani ya miaka mitano malengo yanaweza yasifikiwe.

Ndugai alionyesha wasiwasi wake jana, wakati akisitisha shughuli za Bunge mchana.

"Bima ya afya kwa wote, Kamati ya Huduma za Jamii, msichekecheke, miaka mitano itakwisha, hiyo sheria haijafika hapa bungeni.

"Ni lazima muanze nayo mwanzo, kuanza kufanya ufuatiliaji wa kutosha katika kila hatua, mtoe ushauri wa namna gani jambo hilo linaweza kufanikiwa kwa manufaa ya taifa na wapigakura wetu," alisema.

Alisema yako majukumu ambayo kamati zinapangiwa na Spika, lakini yako majukumu ambayo kamati zinapaswa kujipangia na kuyatekeleza wenyewe kikamilifu, kwa kuwa jukumu lao ni kulishauri Bunge na serikali.

"Niwahakikishie Ofisi ya Bunge iko tayari kutoa ushirikiano na msaada wowote mtakaouhitaji ili kutimiza majukumu yenu kikamilifu," alisisitiza Spika.

Aliwataka wabunge kutoa ushauri wa namna gani jambo hilo linaweza kufanikiwa kwa manufaa ya taifa na wapigakura.

Aidha, Spika Ndugai aliitaka kamati hiyo kusaidia katika masuala ya mabadiliko ya mtazamo katika elimu, akisema kuna haja ya kamati kuonyesha muono wao na kushauri serikali kwenye eneo hilo na si lazima wasubiri mijadala ya kitaifa.

"Kiukweli watoto wetu wanasoma masomo akirudi huna pa kumpeleka, naye hana cha kufanya, kwa nini tusielekeze nguvu zetu nyingi katika maeneo ambayo mtoto anaweza kujiajiri na kuisaidia nchi katika uchumi wa kati," alisema.

HABARI KITAIFA

# Matapeli wa mtandao, matusi kibano chaja

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KIBANO dhidi ya wanaofanya utapeli, wanaotoa lugha za matusi na kukashifu watu kwa njia ya mtandao kimerejea rasmi, baada ya serikali kuanzisha kampeni maalum ya kuwashughulikia.

Hadi kufikia sasa, genge la watu 17 wanaoongoza uhalifu wa mtandao, limekamatwa likiwa limejificha mkoani Morogoro na mitambo yao.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, alisema jana kuwa watu hao watafikishwa mahakamani wakati wowote.

Alikuwa akizungumza jana bungeni jijini hapa wakati wa utiaji saini mikataba minne kati ya wizara yake na makandarasi wa ujenzi, upanuzi na uunganishaji wa mkongo wa taifa wa mawasiliano na miundombinu ya anwani za makazi na postikodi.

“Tumeanzisha kampeni na wale wote ambao wamekuwa wakitoa lugha za matusi, kukashifu watu, kufanya utapeli kwa njia ya mtandao. Tunawachukulia hatua na tutaendelea kuwachukulia hatua wengine. Katika TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) huwezi ukajificha. Utakimbia lakini tutakukamata,” alisema.

Kuhusu madai ya wizi wa vifurushi, Waziri Dk. Ndugulile alisema serikali imedhamiria kutatua tatizo la vifurushi na bando na inataka ifikapo Februari 28, mwaka huu, iwe na majibu ya kudumu.

“Ni lazima tukaangalie, tukakae na zile kampuni, tuangalie ni jinsi gani hatuathiri mapato ya kampuni, hatuathiri mapato ya serikali, lakini vilevile hatumwathiri mwananchi.

“Bado tuna shida kubwa sana ya watu wanatumia mitandao vibaya kufanya utapeli, kukashfu watu na kutukana watu. Nitoe rai mwananchi, mtu yeyote asikupigie simu, akisema ametoka katika kampuni ya simu, wala TCRA (Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania), wala TTCL (Shirika la Mawasiliano Tanzania), akikupa maelekezo ya namna ya kubofya simu yako.

Watu wengi wanaibiwa na watu wasiokuwa waaminifu. Nenda kwenye vituo vilivyosajiliwa na vinavyotambuliwa na kampuni za simu.”

**WASHAURI ELEKEZI ‘OUT’**

Katika kupunguza gharama za washauri elekezi wakati wa utekelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa kilomita 409 za mkongo wa mawasiliano ya taifa, Dk. Ndugulile alisema serikali imewaondoa washauri elekezi kwa sababu gharama ni nyingi na ni kubwa sana.

“Tumesema hizo gharama ni nyingi na mara nyingi zinakuwa kubwa sana. Tuna wataalamu ndani ya wizara na ndani ya taasisi zetu.

“Tumesema hao hao ambao ni wataalamu, tuwatumie badala ya kuwa na washauri elekezi. Hii itatusaidia sana kuokoa fedha nyingi, lakini vile vile itatusaidia kusimamia ubora,” alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Ndugulile, hadi sasa mkongo wa taifa umejengwa kilomita 7,910 na mikataba iliyotiwa saini inalenga kuongeza kilomita zingine 409.

Utekelezaji wa miradi hiyo umetengewa Sh. bilioni 11 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano na halmashauri 12 nchini ndizo zitakazoanza kunufaika na ujenzi huo.

KAMPUNI 4 ZA WAZALENDO

Aidha, Waziri huyo alisema Kampuni ya Raddy Fibre Solution Ltd imeshinda zabuni mbili za ujenzi na upanuzi wa mkongo wa taifa wa mawasiliano.

Itatekeleza mradi wa kwanza utakaochukua miezi minane, ukiwa na kilomita 265 kutoka Manyoni- Singida hadi kambi katoto-Mbeya na mradi wa pili ulipangwa kujengwa kwa miezi sita, una kilomita 72 zilizopo mkoani Mtwara.

Vile vile, wizara hiyo imetia saini mkataba na makandarasi wawili kwa ajili ya kujenga na kuunganisha mkongo wa taifa wa mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini.

Makandarasi hao ni Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL CORP) ambayo imeshinda zabuni ya kujenga miundombinu hiyo yenye kilomita 72 kutoka mji wa serikali wa Mtumba na maeneo mengine ya Jiji la Dodoma. mkataba wake ni wa miezi sita.

# Tume ya RC yabaini dereva wa lori alifariki dunia kwa homa ya mapafu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TUME iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuchunguza utata wa kifo cha aliyekuwa dereva wa lori, Abdulrhaman Issa, imethibitisha kuwa dereva huyo alifariki dunia kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu na si kipigo cha polisi kama ilivyokuwa inadhaniwa awali.

Aidha, tume hiyo imebaini kuwa dereva huyo alifikishwa katika Hospitali ya Igawilo iliyoko Mbeya Mjini akiwa tayari amefariki dunia na kwamba baada ya mwili wake kuchunguzwa haukuwa na majeraha ya aina yoyote yanayoashiria kuwa alipigwa na askari.

Kati ya Januari 27 na 28, video iliyoonyesha purukushani kati ya askari watano wa Jeshi la Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani na dereva huyo ilianza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii kabla ya dereva huyo kuripotiwa kuwa amefariki dunia, huku chanzo halisi kikiwa hakijulikani.

Utata wa kifo hicho ulimsukuma Chalamila kuunda tume ya watu saba kuchunguza tukio hilo ndani ya siku tatu ili kubaini sababu ya kifo hicho huku akizuia mwili wa marehemu kuzikwa mpaka baada ya siku tatu ambazo aliipatia tume hiyo kumaliza uchunguzi.

Tume hiyo iliundwa na maofisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Magereza, Idara ya Uhamiaji, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Usalama wa Taifa na mmoja kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Akitoa taarifa ya tume hiyo ofsini kwake jana, Chalamila alisema tume hiyo ilifanya uchunguzi kwa kuanzia katika Hospitali ya Chimala ambako marehemu alikuwa amelazwa kwa siku moja kabla ya kuendelea na safari.

“Pia tume hiyo ilibaini kuwa mgonjwa alikuwa na historia ya ugonjwa wa pumu maelezo ambayo aliyatoa mwenyewe wakati anasajiliwa katika Hospitali ya Chimala, lakini walipompima alibainika kuwa na maambukizi kwenye mfumo wa mkojo (UTI),” alisema.

Chalamila alisema taarifa ya tume hiyo inaonyesha kuwa baada ya mgonjwa huyo kulazwa Chimala akiwa na mmoja wa ndugu zake waliomba aruhusiwe ili akatibiwe katika Mji wa Tunduma ambako kuna ndugu zao.

Alisema madaktari hao walikubali kumruhusu kwa masharti ya kutoendesha gari, lakini yeye alikaidi na kuchukua gari akaondoka nalo akiwa peke yake bila msaidizi yeyote.

Wakati anaendelea na safari, Chalamila alisema alikuwa anayumbayumba hali iliyosababisha kuyaparamia baadhi ya magari na kufanya wasamaria wema kutoa taarifa kituo cha polisi ili asimamishwe kuepusha madhara.

Alisema askari walimsimamisha mara mbili akagoma na kuendelea na safari na ndipo wakaamua kumwekea kizuizi katika eneo la Inyala ambapo ndipo walipolazimika kutumia nguvu kumshusha kwenye gari baada ya kukaidi kushuka bila shurti.

“Maaskari waliweka kizingiti na ndipo alipokubali kusimama na wakamshusha na kumpeleka lockup (mahabusu), lakini uchunguzi wa tume umebaini kuwa wakati wanamshusha hakukuwa na kipigo cha aina yoyote na wala hakujibamiza,” alisema.

Baada ya kujiridhisha na majibu ya tume hiyo aliamua kuruhusu familia ya marehemu kuuchukua mwili na kwenda kuuzika na kwamba kama haijaridhika na kutaka hatua zaidi mwili huo unaweza ukaendelea kubaki hospitalini kwa ajili ya ushahidi.

Hata hivyo aliagiza Ofisi ya Kamanda wa Polisi ya Mkoa wa Mbeya kugharimia mazishi ya dereva huyo ikiwamo kutafuta gari la kusafirishia kwa maelezo kuwa pamoja na matatizo yake, lakini alifariki akiwa bado yuko mikononi mwa polisi.

Pia aliwataka madereva wa vyombo vya moto waliokuwa wanajiandaa kugoma kufanya kazi kwa sababu ya tukio la kifo cha dereva huyo wakidai alikuwa ameuawa na askari polisi, kuachana na mgomo huo na badala yake waendelee kufanya kazi kwa kuzingatia sheria.


## NOTISI / TANGAZO

**NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEERS AND DEBT COLLECTORS LTD, BEST GROUP LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,MASHOKA AUCTION MART,** kwa Mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha

| JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| ANETH FRANCIS MARABA | ANETH FRANCIS MARABA | NYUMBA | MKURANGA | 31/3/2021 NA KUENDELEA |
| BAHATI JAMES MAGOTI | BAHATI JAMES MAGOTI | NYUMBA | TEMEKE KILUNGULE | 20/2/2021 NA KUENDELEA |
| JUDITH JOVINARY BENEDICTOR | JUDITH JOVINARY ENEDICTOR | NYUMBA | MBEZI-MSINGWA | 10/03/2021 NA KUENDELEA |
| KHAMIS HAJI FAKI | KHAMIS HAJI FAKI | NYUMBA | BUYUNI-MGEULE | 3/3/2021 NA KUENDELEA |
| MALIKI MOHAMED MADIGADI | MALKI MOAMED MADIGADI | NYUMBA | KAZOLE VIKINDU-MKURANGA | 24/2/2021 NA KUENDELEA |
| MICHAEL NDAYUNZE | YADUNIA HAMISI OMARY | NYUMBA | MSONGOLA-MBONDOLE | 24/3/2021 NA KUENDELEA |
| MWAMPYATE LEONARD EDWIN | MWAMPYATE LEONARD EDWIN | NYUMBA | KONGOLO-IGURUSI | 26/02/2021NAKUENDELEA |
| NEEMA JUSTINE MASANJA | MARRY OBADIA MBWILO | NYUMBA NA GHALA LA KUHIFADHIA MAZAO | CHIMALA | 26/02/2021 NAKUENDELEA |
| OMARY YUSUPH HEMEDI | OMARY YUSUPH HEMEDI | NYUMBA | SALASALA-KINONDONI | 17/2/2021 NA KUENDELEA |
| OSCAR IBRAHIM MLIGO | MARY LAZARO SEMITI | NYUMBA | UGOMBOLWA -SEGEREA | 18/2/2021 NA KUENDELEA |
| TIMOTH JULIUS MANYANGU | HARUNI MICHAEL MHAVILE | NYUMBA | CHIMALA | 26/02/2021NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0713077474/0682981090**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki Itarudisha kiasi cha fedha kilicho wekwa na mnunuzi benki bila gharama yoyote.

## Ruvuma sasa kupanda misitu hekta 40,000

**Na Gideon Mwakanosya,**

SONGEA

MKOA wa Ruvuma umelenga kupanda miti ya biashara katika eneo lenye ukubwa wa hekta 40,000 hadi ifikapo mwaka 2025.

Mshauri wa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe, alisema jana kuwa mradi huo unatekelezwa kwa miaka 10 kuanzia mwaka 2015, unatekelezwa kwa kupanda miti maeneo ya serikali kuu, serikali za mitaa, vyuo, shule na vijiji.

Challe ameitaja aina ya miti inayopandwa ni ile ambayo inafaa kwa ajili ya malighafi za viwanda vya mazao ya misitu ambayo ni misindano (pine), milingoti (Eucalyptus) na misaji (teak).

'Hadi kufikia mwaka 2020 jumla ya miti ya biashara iliyopandwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ni hekta 4785, halmashauri zilipanda hekta 425, vyuo na shule hekta 420 na watu binafsi hekta 23,964.

Alisema jumla ya mashamba yote ya miti yaliyopandwa katika kipindi hicho ni hekta 29,194 sawa na asilimia 56.1 ya lengo.

Kwa mujibu wa mshauri huyo Ruvuma inalenga kuanzisha mashamba mapya mawili ya miti ya misaji katika wilaya za Tunduru na Nyasa.

Kwa upande wake Mratibu wa Kuendeleza Programu ya mnyororo wa Thamani wa Mazao ya misitu (FORVAC) Mkoa wa Ruvuma, Marcel Mtunda, alisema wameandaa miche ya miti ya biashara aina ya misaji, pine na milingoni ipatayo 4,000,000 ambayo itapandwa maeneo maalum yaliyotengwa na Mkoa yakiwamo Ifinga, Liuli, Liumbe, Upolo, Mpepo, Kipiki na Kihangamahuka.

Alisema mkoa unatekeleza mradi wa kuongeza thamani mazao ya misitu na nyuki kwa kushirikiana na FORVAC na kwamba mradi unatekelezwa katika wilaya zote tano za mkoa.

# Rais amwapisha Galeba Jaji wa Rufani

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana alimwapisha Zephrine Galeba kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania.

Hafla ya kuapishwa kwa Jaji Galeba ilifanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma, Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, Katibu Mkuu Ikulu Dk. Moses Kusiluka, Majaji wa Mahakama ya Rufani, Majaji wa Mahakama Kuu na viongozi wa taasisi ambazo ni wadau wa karibu wa Mahakama.

Galeba ambaye kabla ya hapo alikuwa Jaji wa Mahakama Kuu, aliapishwa baada ya kupandishwa cheo na Rais Magufuli ikiwa ni kutambua mchango wake wa kuthamini lugha ya Kiswahili ambayo aliitumia kutoa hukumu ya kesi ya mapitio namba 23/2020 kati ya mgodi wa dhahabu wa North Mara na mwananchi Gerald Nzumbi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Magufuli alimpongeza Jaji Galeba kwa kupandishwa cheo na amemtaka kwenda kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na taratibu za Mahakama na kwa kumtanguliza Mungu.

Rais Magufuli alitoa wito kwa Mahakama na Wizara ya Katiba na Sheria kufanya mabadiliko ya sheria na mifumo ya Mahakama iliyorithiwa kutoka kwa wakoloni na ambayo imesababisha hukumu za Mahakama kutolewa kwa lugha ya Kiingereza ambayo haifahamiki kwa Watanzania wengi, ili hukumu hizo zitolewe kwa lugha ya Kiswahili.

Amesema hoja za kuwa Kiswahili hakina misamiati ya kutosha hazina mashiko kwa kuwa mwaka 1999 timu ya wanasheria iliandika kamusi ya sheria na pia lugha hiyo inatumiwa na watu wengi, mataifa na taasisi mbalimbali vikiwamo vyombo vya habari vya kimataifa.

Rais alielezea kutofurahishwa na ucheleweshaji wa mambo unaofanywa na Wizara ya Katiba na Sheria na alimwagiza Waziri Nchemba kufuatilia na kuhakikisha mchakato wa kuwaajiri watumishi 200 wa Mahakama ambao kibali cha kuajiriwa kilishatoka wanaajiriwa.



Rais Dk. John Magufuli akimpongeza Zepharine Nyalugenda Galeba baada ya kumwapisha kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Majaliwa asema hakuna kitu kitakachobaki kutekelezwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imejipanga kukamilisha vipaumbele vyote ambavyo havikukamilika katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Akitoa hoja ya kujadili hotuba ya Rais John Magufuli aliyoitoa wakati akizindua Bunge la 12, Novemba 13, mwaka jana, Majaliwa alisema serikali pia imepanga kusimamia ipasavyo maeneo mapya yaliyoibuliwa kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020.

"Nitumie fursa hii kuliarifu Bunge, kwamba baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais kutolewa, utekelezaji wa maelekezo yake ulianza mara moja kwenye maeneo mbalimbali.

"Hii ni kutokana na ukweli kwamba wizara na taasisi zote za serikali, zilichukua hatua za makusudi kuchambua hotuba hiyo, kuainisha maeneo mbalimbali ya utekelezaji na kuja na mipango ya utekelezaji wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu."

Aidha, aliwasihi wabunge kuziishi ndoto za Rais John Magufuli anayetaka kuona Tanzania inajenga uchumi imara, shindani na unaotengeneza ajira za kutosha kwa Watanzania.

Pia Majaliwa alisema wakati akieleza mbalimbali vinavyotarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Rais Magufuli aliweka bayana kuwa mambo yote muhimu yatakayotekelezwa yamebebwa na ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/25.

Kadhalika, alisisitiza kuwa serikali itaendelea kutekeleza na kusimamia masuala muhimu aliyoyaeleza kwenye hotuba yake ya kuzindua Bunge la 11, Novemba 20, 2015.

Kutokana na maelekezo hayo, serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa ahadi na maelekezo ya Rais Magufuli, aliyoyatoa wakati akizindua Bunge la 12 na Bunge la 11.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, licha ya ukweli kwamba tayari utekelezaji wa masuala mbalimbali umeshaanza kwa kasi kubwa, bado michango ya Wabunge ni muhimu katika kuisaidia serikali kutekeleza kikamilifu vipaumbele vilivyoainishwa kwenye hotuba ya Rais Magufuli ambayo wataijadili kwa siku nne.

Amewahakikishia wabunge hao kwamba michango yao itaheshimiwa, itathaminiwa na itaifanyiwa kazi kwa lengo la kushughulikia kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

### HOTUBA YA JPM NI SEMINA ELEKEZI

Wakichangia mjadala wa hoja za serikali na hasa hotuba ya Rais Magufuli ya kulifungua Bunge, Mbunge wa Chalinze (CCM), Ridhiwan Kikwete, alisema hotuba hiyo ni kama semina elekezi kwa kuwa imegusa kila eneo.

"Kwa sasa nchi, wimbo wake mkubwa ni viwanda, lakini haviwezi kuendelea kama hakuna umeme. Rais anatekeleza mradi wa umeme wa Rufiji ambao utamaliza kabisa tatizo la umeme nchini. Naomba waziri husika ausimamie kikamilifu mradi huu ili kuondoa kilio cha upungufu wa umeme," alisema

Kuhusu kumaliza migogoro ya wananchi katika maeneo ya hifadhi, akitolea mfano Hifadhi ya Taifa ya Saadan (Tanga) na vijiji vya jirani, alimtaka waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii, kumaliza mgogoro huo kwa faida ya pande zote mbili.

### TARURA NGUVU NDOGO

Naye Mbunge wa Same Mashariki (CCM), Anne Kilango Malecela alimpongeza Rais, Magufuli kwa kitendo chake cha kuifanya nchi kwa mara ya kwanza kuendesha uchaguzi mkuu kwa fedha za ndani, jambo ambalo limeiheshimisha nchi.

Pia alieleza kufarikijika kwake na maono ya Rais Magufuli kwenye maeneo ya viwanda, barabara na afya, akisisitiza aungwe mkono kuhakikisha miradi inayogusa maeneo hayo inatekelezwa ipasavyo.

Alisema katika eneo la barabara pamoja na juhudi kubwa za ujenzi zilizofanyika, majimbo yao yanategemea zaidi Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), lakini kwa bahati mbaya wakala huo bado hauna fungu la kutosha kutekeleza miradi yake mingi.

**HABARI KITAIFA**

# Akamatwa kwa madai ya kumiliki kiwanda cha kutengenezea silaha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi mkoani Pwani linamshikilia Shabani Athumani (61) mkazi wa Kwamakocho Kata ya Mandela kwa tuhuma za kumiliki kiwanda cha kutengeneza silaha za kienyeji na vifaa vyake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jana kuwa mtuhumiwa alikamatwa Januari 31, mwaka huu, majira ya saa 1:00 usiku akiwa na mtambo wa kufulia vyuma, chupa tano ndogo zenye baruti, fataki 48, risasi 42 za bunduki aina ya gobole.

Alisema vitu vingine alivyokutwa navyo mtuhumiwa ni paketi ya unga wa kiberiti, mitambo mitatu ya silaha aina ya gobole, mitambo ya kutobolea vifaa vya miti vinavyofungwa kwenye silaha aina ya gobole na kopo moja lenye unga wa tindikali ambao unatumika kuunganisha vyuma vinavyofungwa kwenye silaha aina ya gobole.

Wakati huo huo, Polisi mkoani Pwani linawashikilia watu watatu jamii ya wafugaji kwa tuhuma za kung'oa na kuharibu mazao (miche ya korosho) na kusababisha hasara ya Sh. milioni 50.

Kamanda Wankyo alisema shamba hilo ambalo limeharibiwa mazao ni mali ya Romwald Mukandara na John Biginagwa aliyekuwa mtumishi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani.

Alisema tukio hilo lililotokea Januari 27, majira ya saa 4:00 katika kitongoji cha Rubaya Kijiji cha Diozile Wilaya ya Kipolisi ya Chalinze.

Kamanda Wankyo aliwataja watuhumiwa hao wanaodaiwa kuharibu mazao katika ekari saba za wamiliki hao ni Mtuli Chapalisi, Reuben Oyela na Hamis Chambuli na wengine walioshiriki ambao bado wanatafutwa.

Alisema watuhumiwa wote wako polisi na taratibu zikikamilika watafikishwa mahakamani.

**vitu vingine alivyokutwa navyo mtuhumiwa ni paketi ya unga wa kiberiti, mitambo mitatu ya silaha aina ya gobole, mitambo ya kutobolea vifaa vya miti vinavyofungwa kwenye silaha aina ya gobole na kopo moja lenye unga wa tindikali ambao unatumika kuunganisha vyuma vinavyofungwa kwenye silaha aina ya gobole**

# Madereva walalamikia moto vituo vya magari

**Na Maulid Mmbaga**

BAADHI ya madereva wa usafiri wa umma maarufu kama daladala wamelalamikia wafanyabiashara wanaowasha moto kwenye vituo vya magari yanaposimama yakisubiri abiria na kueleza kuwa ni hatari kwa watu wanaolizunguka eneo hilo.

Mmoja wa madereva hao, Muhidini Fundisha, alisema katika stendi ya Daladala ya Manispaa ya Ilala, kumekuwa na utaratibu wa wafanya biashara kuwasha moto na kupika vitafunwa karibu na sehemu magari yanapo paki.

Alisema magari yanayotumia mafuta ya Petroli hayatakiwi kukaa karibu na moto kwa sababu ya uhalisia wa kimiminika hicho ni rahisi kushika moto kwa haraka jambo ambalo linaweza kusababisha mlipuko na kuleta madhara kwa watu.

"Watu hawa wanatumia moto wa mkaa, vipande vya mbao pamoja na vifuu vitu hivyo vina kawaida ya kurusha cheche na endapo zitadondokea kwenye gari ni rahisi kusababisha maafa kwetu sisi kwa kuunguliwa na magari, lakini itahatarisha usalama wa wanaolizinguka eneo hili," alisema Fundisha.

"Jambo hilo pia linasababisha kero kwa abiria kwani wanakosa sehemu ya kusimama kutokana na kwamba watu hao wameziba asilimia kubwa ya eneo linalotumiwa na wasafiri kusimama wakati wakisubiri usafiri," aliongeza.

Sambamba na hilo la kuziba eneo la abiria, alisema hata ile sehemu ndogo iliyobaki wasafiri wanayoitumia kusimama wanabugudhiwa na moshi unaotokana na kuni zinazochomwa na watu hao.

Aidha, aliwataka wasakatonge hao wasiwashe moto ndani ya stendi hiyo karibu na magari yanaposimama badala yake wapike vitu vyao nyumbani na wavipeleke vikiwa tayari na waendelee na biashara yao, ili kuepusha madhara yanayoweza kusababishwa na moto wanaoukoka katika mazingira hayo.

Mmoja wa wafanyabiashara ndani ya kituo hicho, Anitha Rajabu, alisema wanachokifanya wao ni kujitafutia kipato cha kuendesha maisha yao ya kila siku na shughuli zao zinategemea sehemu yenye idadi kubwa ya watu ndio maana wapo katika eneo hilo.

"Watu wengi hawataki vyakula vya baridi au vilivyopikwa muda mrefu wanahitaji vyakula vya moto ndio maana tunalazimika kuja kuvipika hapahapa ili kukidhi matakwa ya wateja wetu," alisema Rajabu.

**Watu hawa wanatumia moto wa mkaa, vipande vya mbao pamoja na vifuu vitu hivyo vina kawaida ya kurusha cheche na endapo zitadondokea kwenye gari ni rahisi kusababisha maafa kwetu sisi kwa kuunguliwa na magari, lakini itahatarisha usalama wa wanaolizinguka eneo hili**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA**

## ORODHA YA MAJINA YA WANUFAIKA WA UFADHILI WA MAFUNZO YA KUENDELEZA UJUZI KWA MAKUNDI MAALUMU NA VIJANA WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU

**1. Utangulizi**

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (5)1 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu Namba 8 ya Mwaka 2001, ili kusimamia Mfuko wa Elimu wa Taifa ulioanzishwa chini ya Sheria hiyo. TEA inatekeleza majukumu yake chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mwaka 2017, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliipatia TEA jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zote zinazohusu utekelezaji wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi kwa lengo la kuzalisha ajira (ESPJ) unaotekelezwa na Wizara hiyo ukipata ufadhili toka Benki ya Dunia. Programu ya ESPJ ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ujuzi (National Skills Development Strategy-NSDS: 2016-2021).

Maeneo muhimu yanayolengwa katika utekelezaji wa programu ya ESPJ ni kuongeza ufanisi katika uzalishaji na pia kuongeza uwiano wa wataalam wa fani mbalimbali katika Sekta sita za kipaumbele (Kilimo na Kilimo Biashara, Utalii na huduma za Ukarimu, Nishati, Ujenzi, Uchukuzi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano-TEHEMA) zenye mchango mkubwa wa kiuchumi nchini.

Ili kuwafikia watanzania wengi zaidi hasa wenye mahitaji ya ujuzi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania imeanzisha Mpango wa Ufadhili (Bursary Scheme) ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi. Mpango huu umelenga kuwezesha mafunzo ya ujuzi kwa vijana kutoka makundi maalum na wanaoishi katika mazingira magumu ili wapate uwezo wa kujishughulisha katika shughuli mbalimbali za uzalishaji zenye tija. Tangazo la kukaribisha maombi ya ufadhili lilitangazwa mapema mwezi Septemba 2020 katika magazeti na tovuti ya TEA.

**2. Muda wa Utekelezaji wa Mpango wa Ufadhili**

Mpango wa ufadhili utatekelezwa kwa muda wa miaka miwili (2) kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2021/2022 kwa kuzingatia programu zilizolengwa.

**3. Muda wa Mafunzo**

Mpango huu unafadhili mafunzo ya muda mfupi kwa kipindi cha kuanzia mwezi mmoja (1) hadi miezi sita (6); na mafunzo ya muda mrefu ya miezi kumi na mbili. Mpango huu hautafadhili mafunzo zaidi ya muda uliotajwa.

**4.Orodha ya Waombaji watakaopatiwa ufadhili.**

Baada ya kupokea na kupitia maombi yaliyotumwa kuomba ufadhili, jumla ya wanufaika 2,102 wamekidhi vigezo vya kupatiwa Ufadhili wa Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi Kwa Makundi maalumu na Vijana wanaoishi katika mazingira magumu. Orodha ya wanufaika imetangazwa katika tovuti ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (www.tea.or.tz) na mbao za matangazo za Halmashauri nchini kote.

**5. Maulizo na Malalamiko**

Waombaji au wanufaika wa ufadhili kama watakuwa na maswali au malalamiko yoyote kuhusu ufadhili huu watapaswa wayawasilishe kwa Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa anwani iliyoonyeshwa hapo chini.

**6. Mawasiliano**

Kwa ufafanuzi au maelezo zaidi wasiliana na: Mratibu wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi kwa Namba ya simu: **0789304181** au Ofisa wa Mpango wa Ufadhili kwa Namba ya simu: **0718744385** au tuma barua pepe kwa: **sdf@tea.or.tz.**

**Imetolewa na:**

**MKURUGENZI MKUU**
**na**
**MSIMAMIZI WA MFUKO WA KUENDELEZA UJUZI (SDF Fund Manager),**
**MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA,**
**S.L.P 34578, DAR ES SALAAM.**
**Barua pepe:info@tea.or.tz,**
**sdf@tea.or.tz | dg@tea.or.tz**

## MAONI & UCHAMBUZI

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# *Urejeshaji kodi za majengo, mabango usimamiwe ipasavyo*

SERIKALI juzi ilitangaza kurejeshwa kwa ukusanyaji wa kodi za mabango na ushuru wa mabango kwa mamlaka za serikali za mitaa baada ya kuziondoa na kuzipeleka Mamlaka ya Mapato Tanzania mwaka 2006.

Kutokana na uamuzi huo, serikali imewataka wakurugenzi wa mamlaka hizo kusimamia makusanyo hayo ili kuongeza mapato ndani ya halmashauri, hivyo kuongeza mapato ya serikali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, alisema kurejeshwa kwa kodi hizo ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuwa wamiliki wa majengo watafikiwa kwa urahisi na halmashauri na pia mabango mengi yako katika maeneo ya mamlaka za mitaa, hivyo kazi itakuwa rahisi kwa ukusanyaji.

Pia alisema kutokana na uamuzi huo, wakurugenzi wa halmashauri zote 185 nchini wamepewa mamlaka za kukusanya kodi hizo na kuhakikisha majengo yote yanalipiwa kodi na kwamba mamlaka hizo zina uwanja mpana wa kuwafikia wenye majengo.

Jafo hakuuma maneno wala kupepesa macho kwamba utekelezaji wa suala hilo unatarajiwa kuanza mara moja huku akionyesha wazi kwamba halmashauri zitaongeze wigo wa makusanyo ya ndani.

Ni kweli kwamba serikali ilipochukua uamuzi wa kuondoa kodi hizo katika halmashauri, ilikuwa na nia nzuri ya kuongeza mapato katika mfuko mkuu wa serikali, lakini sasa imeona kazi hiyo irejeshwe kwa mamlaka hizo kwa ufanisi zaidi.

Kwa mantiki hiyo, tunatumaini kwamba kutakuwa na ukusanyaji wenye tija katika kodi hizo na halmashauri zitakuwa na uwezo wa kifedha hivyo kuhudumia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Pamoja na hatua hiyo, ni vyema pia suala la watumishi wasio waaminifu katika ukusanyaji mapato likaangaliwa kwa jicho la kipelee, ili isionekane kwamba ni sherehe kwao kwa kuwa watapata fedha bila kutumia jasho jingi.

Kinachotakiwa ni kuhakikisha watumishi hao wanamulikwa ipasavyo kwani wakiachiwa wanaweza kutengeneza mianya ya upotevu wa mapato.

Katika maeneo ya halmashauri kuna miradi mingi inayopaswa kutekekezwa kama vile ujenzi wa vituo vya afya na zahanati, elimu, maji na barabara, hivyo fedha nyingi zinahitajika na miongoni mwa vyanzo ni makusanyo hayo.

Usimamizi mzuri wa makusanyo hayo ni chachu kwa maendeleo chanya katika utekelezaji wa baadhi ya miradi hiyo ambayo ni mkombozi wa wananchi. Ni vyema madiwani wakasimamia kwa ukamilifu jambo hilo vinginevyo linaweza kusababisha shida kwao na baadhi ya watendaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# *Mgombea binafsi akiruhusiwa, ni mapokeo ya hodi viongozi vijana*

**KUWAPO** mgombea binafsi nchini, ni miongoni mwa mambo ambayo wadau wa siasa wamekuwa wakitamani, lengo ni kuruhusu wasio katika vyama waweze kuwania nafasi za uongozi.

Marehemu Mchungaji Christopher Mtikila, kiongiozi wa Chama cha DP, alikuwa mwanasiasa aliyetamani kuona Tanzania, inaruhusu mfumo huo, ili wananchi wenye uwezo wa kuongoza wachaguliwe na wananchi, bila ya kuzingatia vyama watokavyo.

Katika harakati zake za kutaka kuwapo mgombea binafsi, mwanasiasa huyo enzi za uhai wake, alifika hadi mahakamani. Pia aliwahi kutangaza kuwa hata chama chake kisingempitisha, angewania urais kama mgombea binafsi, katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010.

Mchungaji Mtikila alifariki dunia kabla hoja yake hiyo ya kutaka mgombea binafsi haijazaa matunda, ingawa miaka ya hivi karibuni mjadala huo umeibuka upya kwenye mitandao ya kijamii.

Ni mjadala uliotokana na wimbi la madiwani na wabunge kuhama vyama na kusababisha kurudiwa kwa uchaguzi, hali inayodaiwa kama kungekuwapo mgombea binafsi gharama za kurudia uchaguzi zingeepukwa.

Wadau hao wa siasa wanaamini kwamba, mfumo wa mgombea binafsi pia unaondoa ukiritimba wa watu kuchaguana kwenye vyama kwa kujuana na kupitishwa bila kupingwa.

Vilevile ni fursa ya kuondoa chuki za kivyama, kwa madai kwamba, hivi sasa watu wanabaguana hadharani na kuonyesha chuki kwa sababu tu ya kuegemea chama fulani.

Mfumo wa mgombea binafsi, unatajwa kuwa njia ya kuwapa nafasi vijana wengi kujitokeza kugombea uongozi, pasipo vikwazo vinavyowekwa na wanasiasa wasiotaka kung'atuka.

Suala hilo na mgombea binafsi, pia linapigiwa debe na kada za Chama Cha Mapinduzi (CCM), Thomas Ngawaiya, anayekumbusha historia ilivyokuwa kabla ya mfumo huo kuondolewa.

Anasema, mwaka 1960 Tanganyika iliruhusu mgombea binafsi katika uchaguzi mkuu ambao TANU ilishinda viti 70 kati ya viti 71 vya ubunge, huku kimojawapo kikiwa ni cha Jimbo la Mbulu mkoani Arusha.

Katika ufafanuzi wake, anasema kiti hicho cha ubunge, kilichukuliwa na mgombea binafsi Herman Sarwatt aliyemshinda mgombea wa TANU, jina la Chifu Amri Dodo.

Hata hivyo, anasema siku chache baadaye, Sarwatt alijiunga na TANU, hivyo utaratibu wa mgombea binafsi ukaondolewa rasmi, kutokana na mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri.

Ngawaiya, aliyekwishapitia uanachama wa vyama vya NCCR Mageuzi, TLP na CCM, pia historia ya kuwahi kuwa mbunge, anaeleza imani yake kwamba si jambo la ajabu yeye kuunga mkono mgombea binafsi, akidai unalenga kumsaidia kila Mtanzania mwenye sifa za kuongoza, apate nafasi hiyo.

Kwa hali hiyo, ni wazi kwamba kile kilichoanzishwa na Mchungaji Mtikila na sasa kinaendelezwa na wadau, hakina budi kudumishwa, ikiwa sehemu ya kuimarisha demokrasia nchini.

Ni zao la ukweli, wapo baadhi ya vijana wanaotamani kupata uongozi na huenda wanakwama kutokana na mfumo unaowalazimu kupitia kwenye vyama, ambako wakati mwingine wanakumbana na shida.

Anataja kuwa ni njia pekee inayowawezesha Watanzania washike nafasi mbalimbali za uongozi, vinginevyo wengi wataendelea kukwama kuongoza kwa sababu tu ya mfumo wa kupitia katika vyama vya siasa.

Ndiko iliko imani ya kisiasa kwa wadau wanashauri kuwapo mgombea binafsi, kwa mtazamo wa kupanua wigi wa kupata viongozi bora zaidi na si kuishia kuwa na wanasiasa tu.

Muungwana naungana na mawazo hayo, kwa sababu inawezekana wapo watu wengi ambao si wanasiasa na wanaotamani kuongoza na wanakwamishwa na mfumo uliopo wa kupitia kwenye vyama.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Doroth Ngwajima (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kukomeshwa kwa unyanyasaji wa kijinsia kwa makundi yote. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Gwajima ataka wanaume kupaza sauti kuhusu kufanyiwa ukatili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka wanaume wanaofanyiwa vitendo vya ukatili kuripoti kwa mamlaka zinazohusika bila kuona aibu ili hatua stahiki zichukuliwe.

Aidha, imewaagiza maofisa ustawi wa jamii kwenye halmashauri nchini kushughulikia ipasavyo vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake, wanaume, watoto na wazee kwenye maeneo yao na kuchukua hatua kwa wakati.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kuhusu vitendo vya ukatili katika jamii.

Alisema wanaume wamekuwa na tabia ya usiri na wavumilivu na wakati umefika kwa wao kuvunja ukimya na kuripoti vitendo vya ukatili vinavyofanywa dhidi yao.

Hata hivyo, alisema wataangalia uwezekano wa kuwasikiliza wanaume peke yao kama wanaona kuna vikwazo vya wao katika kuwasilisha vitendo wanavyofanyiwa.

"Wanaume waache kukaa kimya dhidi ya vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa, toeni taarifa mapema kwa mamlaka zinazohusika ili mpate msaada mapema ili kuzuia madhara zaidi kutokea," alisema.

Aliwataka maofisa hao kusimamia utekelezaji wa maagizo yake ya kushughulikia ipasavyo ukatili dhidi ya wanawake, wanaume, watoto na wazee na kuhakikisha haki za wananchi wanaoonewa ikiwamo makundi tete zinapatikana kwa wakati.

"Mtakumbuka mnamo Januari 29, 2021 nilitoa tamko kuhusu kuongezeka kwa vitendo vya ukatili ikiwamo mauaji katika familia katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, nilitoa tamko hilo baada ya kuona vitendo vya ukatili vinazidi kuongezeka kila kukicha," alisema.

Alitaja miongoni mwa matukio yaliyotokea hivi karibuni ni pamoja na baba mmoja mkazi wa Kinondoni jijini Dar es Salaam aliwekwa mbaroni akidaiwa kumkata mapanga mkewe baada ya kushindwa kumrubuni mkewe huyo awanyweshe sumu watoto wao wawili ili wafe.

"Pia Januari 20, wilayani Shinyanga mama alimuunguza mtoto wake kwa jiko la mkaa kwa sababu ya kuunguza mboga, Januari 21, mwaka huu, iliripotiwa baba kumfinya mtoto kwa plaizi kisa kutojua kusoma na kuandika, huko huko Shinyanga. Pia kuna taarifa ya baba kumbaka binti yake wa miaka 11 wilayani Serengeti, taarifa iliyoripotiwa Januari 23 mwaka huu," alisema.

Kadhalika, alisema tukio lingine lilitokea Manispaa ya Shinyanga Januari 26, mwaka huu, kwa mwanamke mwenye umri wa miaka 30 kupigwa kwa mchi wa kinu kichwani na mumewe na kufariki dunia baada ya kutokea ugomvi wa kifamilia.

Hata hivyo, alisema wizara imepata mwitikio mkubwa kutoka kwa wananchi wakiguswa sana kuhusu vitendo hivyo, na kueleza kuwa vitendo hivyo vimekuwa vikifanywa si tu kwa wanawake na watoto, bali vimekuwa vikifanywa pia kwa wazee na makundi mengine katika kijamii.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau imejitahidi kutokomeza mauaji dhidi ya wazee hapa nchini, bado vitendo vya ukatili vinaendelea katika maeneo kadhaa hapa nchini, hivyo basi, niwahakikishie kuwa serikali inaendelea na mapambano dhidi ya vitendo hivi ili kuhakikisha vinakwisha kabisa," alisema.

Alisisitiza kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kutokomeza Mauaji dhidi ya Wazee (2018/19 - 2022/23) na Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017 - 2022).

Dk. Gwajima alisema vitendo hivyo vya ukatili vinaashiria uwepo wa migogoro ya kifamilia inayotokana na sababu mbalimbali ikiwamo kugombania mali, matatizo ya kisaikolojia ambayo hayapatiwi ufumbuzi mapema na jamii kutokutekeleza wajibu wake wa kutunza na kuimarisha ulinzi kuanzia ngazi ya familia.

Alitoa wito kwa familia, jamii na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kushirikiana katika kufichua vitendo vya ukatili katika jamii na kubaini mapema viashiria vyake ili kuwezesha upatikanaji wa haki kwa wakati.


## MAJEMBE AUCTION MART LTD
## (VIJANA WA KAZI)

# NOTISI/MNADA:

KWA NIABA YA **DIGITAL AUCTION MART LIMITED,** TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA WADAIWA WALIOTAJWA HAPA CHINI WALIPE MADENI YAO WANAYODAIWA NA **DIGITAL AUCTION MART LIMITED.**

ENDAPO WATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA, DHAMANA ZAO (VIWANJA) ZITAUZWA KWA MNADA WA HADHARA KWA RATIBA IFUATAYO:-

| NA. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA/SIFA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | KELVIN KIDEKA IDD | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,SHIRIKISHO,BLOCK D – PLOT NO 11 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 2 | DEOGRATIUS ATILYO KALINGA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,SHIRIKISHO,BLOCK D – PLOT NO 17 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 3 | BERNARD VICENT NYAMGOYE | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,SHIRIKISHO,BLOCK D – PLOT NO 26 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 4 | KELVIN HASHIL NDYALI | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,SHIRIKISHO,BLOCK D – PLOT NO 33 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 5 | YUSUFU MUSA WASHOKERA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO I,BLOCK D – PLOT NO 7 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 6 | RAMLA SALEH SURUR | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO I,BLOCK D – PLOT NO 8 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 7 | CAROLYNE JONES MSOKWA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO I,BLOCK D – PLOT NO 9 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 8 | MAGRETH RESPICE LYARUU | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO I,BLOCK D – PLOT NO 47 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 9 | REVOCATUS YOLONIMO MAGEZI | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 64 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 10 | NEEMA ALPHAXARD BWAIRA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 05 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 11 | NEEMA ALPHAXARD BWAIRA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 6 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 12 | JESSY PAUL MPANGALA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 18 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 13 | JANE FREDRICK PELEZI | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 35 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 14 | JUDITH JASTUS ISSACK | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 42 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 15 | ELIZABETH CHARLES MASOLWA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 51 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 16 | KENNEDY YUSUFU ANDREA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 60 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 17 | FADYA JUMANNE FEREJ | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 61 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 18 | HAMZA JANGALE CHOME | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 69 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 19 | FELIX DOMINIC MLAY | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 75 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 20 | ISACK JULIUS RYOBA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 94 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 21 | ROGER TIMOTH KOMBA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 101 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 22 | ZACHARIA MARTIN PHILIP/HELLE | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 102 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 23 | ZACHARIA MARTIN PHILIP/HELLE | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 103 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 24 | SAID KHALFAN OMARY | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 111 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 25 | LAURIAN GLORIA LEONCE | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 123 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 26 | RODNEY TUMAINI LEONCE | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 124 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 27 | BRIAN FRANCIS SABATELE | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 138 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 28 | ALOYCE JOHN MROSSO | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 144 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 29 | ISAYA FESTO KAPINGA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 146 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 30 | FRANCIS GERALD MHINA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 152 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 31 | FRANCIS GERALD MHINA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 153 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 32 | FELICHISMO JOHN MALLYA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 173 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 33 | MOSES MATHIAS MAKARIUS | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 175 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 34 | AISHA ALLY KAMBON | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 190 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 35 | MOSES MANENO MLAWA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 200 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 36 | ABUUBAKARI AGIBU DIMANDO | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 211 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 37 | SIE YUNGA MTINDA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 212 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 38 | DONAWEDA EPIPHANY MASSAWE | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 213 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 39 | DONROGERS EPIPHAN KMAKAZI | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 214 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 40 | DONROGERS EPIPHAN KMAKAZI | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 215 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 41 | STELLA ANDREW MHENGA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 216 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 42 | MBAZI ALLEN SHEKWAVI | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 218 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 43 | SHABAN DAUD SHABAN | VIWANJA–VIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 224 NA 225 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 44 | ZAHOR SULEIMAN MZUZURI/ASI | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 229 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 45 | MATHEW LEO KASONTA | VIWANJA–VIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 233 NA 234 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 46 | ISSA HASSAN CHIPATAGA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 236 | IJUMAA 12.02.2021 |
| 47 | AHMADA RAMADHANI MPWANA | KIWANJA–KIPO KIGAMBONI,LINGATO II,BLOCK D – PLOT NO 238 | IJUMAA 12.02.2021 |

**MASHARTI YA MNADA:**

A). UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.

B). MALIPO NI 25% YA BEI ITAKAYOFIKIA KWENYE MNADA NA SALIO LITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) TU.

C). ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOTOLEWA, ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE ZOTE NA NYUMBA ITAUZWA TENA.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NA. 0754/84/13-301930,0715868000 NA 0745707008**

# Mwenyekiti BOA atembelea matawi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Benki ya Afrika (BOA) Tanzania, Dk. Nyamajeje Weggoro, ameanza kutekeleza mkakati wa kuendeleza benki kwa kutembelea matawi makubwa mawili.

Matawi aliyotembelea ni Business Center, Oysterbay, tawi ambalo ni kituo kikubwa cha kutoa huduma kwa wateja wa kampuni na biashara na tawi la Victoria lililoko Kijitonyama.

Ziara hii inafanyika baada ya mwenyekiti kukutana na uongozi na wafanyakazi wa benki hiyo katika makao makuu ya benki hiyo yaliyoko kwenye jengo la NDC na kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusiana na kuboresha uendeshaji wa benki kwa ufanisi zaidi.

Dk. Weggoro alitembelea matawi kuelewa shughuli za benki katika kusaidia maendeleo ya nchi na mchango wake katika kukuza ujumuishaji wa huduma za kifedha hususani kipindi hiki ambacho Tanzania imeingia katika uchumi wa kati.

Benki hiyo imeonekana kuwa thabiti katika kufanikisha uwekezaji uliofanywa nchini Tanzania na imeshiriki katika miradi mbalimbali ya maendeleo tangu 2007.

Pamoja na ushiriki wa benki hiyo katika miradi mbalimbali ya maendeleo, benki imeonyesha dhamira yake katika kusaidia biashara ndogo na za kati (SME) kwa kubuni bidhaa na huduma za kuvutia wateja.

Ikiwa benki ya biashara, inayo wateja waliogawanywa katika makundi ya wateja wa rejareja, biashara ndogo na za kati (SME) na wateja wa kampuni.

Kabla ya kujiunga na BOA Tanzania, Dk. Weggoro, aliteuliwa kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Benki ya Maendeleo ya Afrika kati ya mwaka 2016 hadi 2019.

Pia alifanya kazi kwa weledi mkubwa akisimamia maslahi ya nchi nane za Tanzania, Kenya, Uganda, Ethiopia, Rwanda, Eritrea, Visiwa vya Shelisheli, na Sudan Kusini.

# Wadaiwa sugu NHC kikaangoni

**Munir Shemweta,**
SHINYANGA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) linatarajia kuanza uchambuzi kwa wadaiwa sugu wa nyumba zake katika mikoa 24 ya Tanzania Bara, ili kuchukua hatua za kisheria dhidi yao.

Uamuzi huo unatokana na wadaiwa muda waliopewa kukamilisha malipo ya malimbikizo kumalizika Januari 31, mwaka huu.

Meneja Uhusiano na Huduma za Jamii wa (NHC), Muungano Saguya, alisema hayo juzi mkoani hapa wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi, kuhamasisha ukusanyaji kodi ya ardhi na kukagua miradi inayotekelezwa na NHC.

Alisema baada ya NHC kutoa muda wa mwezi mmoja hadi Januari 31, wapangaji wake wanaodaiwa malimbikizo ya kodi ya pango la nyumba wawe wamelipa kodi hiyo, NHC sasa inafanya uchambuzi katika mikoa yenye nyumba hizo kwa lengo la kuhakikisha kila mkoa unapeleka taarifa sahihi za wapangaji waliokaidi kutekeleza agizo ili kuchukuliwa hatua.

"Kwanza tunawashukuru wale wapangaji waliolipa malimbikizo ya kodi lakini wasiokamilisha malimbikizo, shirika letu litachukua hatua stahiki za kuwanyang'anya nyumba na kuwapatia watu wengine wanaozihitaji," alisema Saguya.

Kwa mujibu wa Saguya, kuna idadi kubwa ya wananchi wanaohitaji nyumba za shirika, lakini baadhi ya waliopewa fursa za kuzitumia nyumba hizo wamekuwa wagumu kulipa kodi na shirika litachukua hatua za kuwanyang'anya.

Saguya aliongeza kuwa kutokana na kutofanya vizuri kwa baadhi ya kampuni zilizopewa kazi ya upangaji miji katika maeneo mbalimbali na halmashauri, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kulitumia shirika lake katika kazi hiyo kwa kuwa lina mamlaka ya kupanga miji.

Sambamba na hilo, alisema NHC mbali na kujenga nyumba na kupangisha katika maeneo mbalimbali kama ujenzi wa takriban nyumba 50 katika katika Wilaya ya Kahama, alitoa wito kwa halmashauri kulitumia kujengewa nyumba za watumishi.

Alitaja baadhi ya mambo ambayo NHC inahitaji kabla ya kupewa kazi ya ujenzi wa nyumba ni ardhi isiyo na fidia, eneo lenye miundombinu na uhakika wa kupatiwa malipo kwa kuwa shirika hilo ni la kibiashara na halipati ruzuku ya serikali kwa kuwa linahitaji uwekezaji wenye tija.

Aidha, Saguya alisema shirika lake linajenga pia majengo ya taasisi kama mkandarasi wa daraja la kwanza na kusisitiza kuwa halmashauri zinaweza kulitumia shirika hilo hata kama siyo kujenga nyumba za kununua bali kujenga majengo.

Kwa sasa NHC inatekeleza miradi ya ujenzi wa zaidi ya nyumba 44 za Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) katika maeneo mbalimbali sambamba na ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini eneo la Mikindani Mtwara na Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Musoma maarufu Kwangwa.

Miradi mingine ni ujenzi wa ofsi za wilaya za Wanging'ombe Mkoa wa Njombe, Malinyi Mkoa wa Morogoro na Hai mkoani Kilimanjaro na kusisitiza wakurugenzi wa halmashauri kuendelea kulitumia shirika.



Mkurungenzi Mkuu kampuni tanzu ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Joseph Challo (kushoto), akipokea mkataba wa makubaliano ya kusambaza vibao vya kuonyesha majina ya barabara na namba za makazi (Post code) nchini, kwa niaba ya Serikali kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari, Dk. Zainabu Chaula (katikati), jijini Dodoma jana. Anayeshuhudia ni Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Faustine Ndugulile. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TFS yaanza utekelezaji agizo la Rais Magufuli

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), umesema umeanza kufanyia kazi kwa haraka agizo la Rais John Magufuli la kuhakikisha magogo hayauzwi nje ili taifa lisiendelee kupoteza mapato.

Katika kuhakikisha utekelezaji huo unakuwa wa thamani, TFS imesema itaongeza mbao thamani na kutengeneza samani ambazo ndizo zitasafirishwa.

Kamishna Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, aliyasema hayo ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana ikiwa ni siku chache tangu Rais Magufuli alipozindua Shamba la Miti la Silayo lililoko Chato mkoani Geita.

"Tutashirikiana na taasisi za serikali likiwamo Jeshi la Magereza, SUMA JKT, Kikosi cha JWTZ Mzinga na Shirika la Taifa la Nyumba (NHC) na watu binafsi wenye viwanda kuzalishe bidhaa za samani ambazo zitasafirishwa nje," alisema Prof. Silayo.

Pia alisema kwa sasa hapa nchini kuna uwekezaji mkubwa wa viwanda bidhaa za hapa kusafirishwa nje kwenda katika nchi za Rwanda, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Pia alisema Kiwanda cha Nguzo za Umeme Mafinga kimesaidia nchi yetu kutoagiza nguzo za umeme kutoka nje.

Katika hatua nyingine, Kamishna Silayo alisema TFS ina deni kubwa la kulipa kwa Rais Magufuli kutokana na imani kubwa aliyo nayo kwao kwa kuhakikisha misitu inakuwa salama.

Prof. Silayo alisema sekta ya misitu ina mchango mkubwa katika uchumi wa Tanzania na kwamba Rais Magufuli anataka kuona maendeleo ya taifa na wananchi yanafikiwa kwa haraka, na kuwa TFS kupewa sifa ni changamoto kubwa kwake na wafanyakazi wote kwa kuhakikisha wanaongeza bidii katika utendaji kazi.

"Nawashukuru askari wetu wa TFS na wafanyakazi wote, mafanikio yetu ni mchango wa kila mmoja wetu na Rais ameutambua utendaji wetu. Hata hivyo, hii ni changamoto ambayo Rais Magufuli ametupa hivyo tufanye kazi kwa bidii na weledi na kuimarisha ushirikiano," alisema Prof. Silayo.

Alisema Rais anatarajia TFS ifanye kazi kwa bidii zaidi, hivyo ni jukumu la kila mmoja atambue kuwa hapaswi kurudi nyuma na badala yake aongeze kasi katika utendaji wake.

# EWURA yadhibiti uchakachuaji mafuta

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepambana na kupunguza tatizo la uchakachuaji wa mafuta kutoka asilimia 80 mwaka 2007 hadi asilimia nne mwaka jana.

Hayo yalisema jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, wakati wa mkutano wa kiufundi na uhamasishaji kwa waandishi wa habari Kanda ya Ziwa juu ya masuala ya udhibiti wa huduma za nishati na maji, ulioandaliwa mamlaka hiyo na kufanyika mjini hapa.

Mhandisi Chibulunje alisema suala la uchakachuaji wa mafuta nchini limekuwa tatizo, lakini EWURA wamepambana na kupunguza kwa asilimia kubwa.

Alisema EWURA inadhibiti ubora wa miundombinu ya mafuta ili kulinda afya, usalama na mazingira ambapo kutokana na udhibiti huo maghala na vituo vya mafuta vimeendelea kuwa bora zaidi.

Pia alisema imeandaa masharti nafuu ili kuvutia wawekezaji kwenye maeneo ya vijijini pamoja na kutoa mwongozo wa ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini kwa gharama nafuu.

Sambamba na hayo, Chibulunje alisema EWURA inatoa leseni ili kuhakikisha huduma za mafuta zinatolewa kwa kufuata sheria, kanuni na viwango stahiki hadi kufikia Juni, mwaka jana, imetoa leseni 1,515 katika sekta ya mafuta, kati ya hizo leseni 58 ni za kuuza mafuta kwa jumla.

Chibulunje alisema mamlaka hiyo imeandaa mfumo wa kuuza mafuta vijijini kwa kutumia vituo vinavyotembea ili kuongeza upatikanaji wa mafuta kwa njia ambazo ni salama na inayozingatia utunzaji wa mazingira.

Pia alisema mfumo huo utaondoa utunzaji na uuzaji wa mafuta kwenye mapipa, madumu na chupa za plastiki.

Naye Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, aliwataka waandishi wa habari waliopata elimu hiyo kuwa mabalozi kwa kusaidia kufikisha elimu kwa jamii kupitia taaluma yao na waendelee kushirikiana pamoja.

# Hospitali ya Kairuki yamkumbuka mwanzilishi wa kupima afya bure

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya Kairuki iliyoko Mikocheni jijini Dar es Salaam, imepanga kutoa huduma ya upimaji afya bure ikiwa ni kumbukumbu ya mwanzilishi wa hospitali hiyo, Prof. Hurbert Kairuki.

Uzinduzi wa huduma hizo za upimaji bila malipo zinatarajiwa kufanyika leo katika kituo kipya cha mabasi Mbezi Luis. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa hospitali hiyo, Arafa Juba, shughuli hizo zinafanywa kumkumbuka Prof. Kairuki ambaye pia ni mwanzilishi wa Mtandao wa Shirika la Afya na Elimu (KHEN), aliyefariki Februari 6, 1999.

Arafa alisema huduma mbalimbali za kumbukizi ya Prof. Kairuki zitafanyika kuanzia leo hadi keshokutwa na baadhi ya huduma zitakazokuwa zikitolewa ni pamoja na kupima watu wenye uoni hafifu.

Mkuu huyo alisema watawapima watu mbalimbali ugonjwa wa kisukari, uwiano wa urefu na uzito, shinikizo la damu, kutoa elimu ya lishe na uchunguzi wa awali kwa wenye uvimbe kwenye matiti.

Alisema wataalamu wa hospitali hiyo watawapa ushauri wa kitaalamu watu mbalimbali watakaofika kwenye upimaji na kwamba kutakuwa na uchangiaji wa damu kwa hiyari.

"Pia tutahamasisha watu wajiunge na bima ya afya iliyoboreshwa (CHF), kituo kipya cha mabasi Mbezi Luisi, hivyo wananchi wajitokeze kwa wingi kwasababu huduma zote hizi zitatolewa bure na tunafanya kila mwaka kumuenzi," alisema Arafa. Alisema Prof. Kairuki licha ya kuwa mwanzilishi wa hospitali hiyo ni mwanzilishi wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) na Shule Kuu ya Uuguzi ya Kairuki.

Arafa alisema pia Prof. Kairuki ni mwanzilishi wa Mtandao wa Shirika la Afya na Elimu (KHEN), ambapo pia umeanzisha kiwanda cha kutengeneza dawa (Kairuki Pharmaceuticals Industry) kilichoko Zegereni, Kibaha.

"Kiwanda hiki kiko kwenye maandalizi ya mwisho na kitazinduliwa wakati wowote. Haya ni matunda ya mwanzilishi wetu Profesa Kairuki hivyo tunakila sababu ya kumuenzi kwa matukio mbalimbali kama kutoa huduma za afya bure," alisema Arafa




Mwenyekiti wa Bodi Benki ya Afrika, Dk. Nyamajeje Weggoro (kushoto), akijadiliana jambo na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Wasia Mushi (katikati) na Mkuu wa kitengo cha kuhudumia wateja wadogo, Lomnyaki Saitabau, alipofanya ziara ya kikazi katika tawi la Victoria, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC, TPSF wajadili fursa zilizoko SGR

**Na Jumanne Juma**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) na Taasisi ya Sekta Binafsi ya Tanzania (TPSF), wameandaa jukwaa la majadiliano ya jinsi gani wadau wa sekta hiyo watachangia na kufaidika na mradi wa reli ya kisasa.

Jukwaa hilo lililofanyika jijini Mwanza na kushirikisha wanachama wa TPSF, NBC, Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Kampuni ya Ujenzi la Uhandisi la China (CCECC) ili kujadili ushiriki wa sekta binafsi katika kufanikisha na kukamilisha mradi wa SGR.

Kwa mujibu wa taarifa ya NBC , ilisema inaendelea kutoa mchango mkubwa katika sekta binafsi ili kuhakikisha malengo na jitihada za serikali ya kukuza ushiriki wa sekta binafsi katika miradi mikubwa ya kimkakati ya kitaifa.

Lengo kubwa la jukwaa hilo ni kuanzisha uhusiano mzuri wa kibiashara na kazi biana ya (CCECC) mkandarasi mkuu wa mradi huu na wadau wa sekta binafsi, kubadilishana uzoefu na kuhimiza ushirikiano, kutambua na kuthibitisha jukumu muhimu la sekta binafsi kama injini ya ukuaji wa uchumi wa nchi, pamoja na kuimarisha ushirikiano wa umma na sekta binafsi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Ofisa Uhusiano kwa Wateja Wadogo na wa Kati NBC Tawi la Mwanza, Esther Kahabi, alisema benki hiyo ina uzoefu wa zaidi ya miaka 50 katika kuhudumia wateja wadogo na wa kati.

"Tuna bidhaa mpya za mikopo zilizoanzishwa mahususi kulenga wakandarasi na wazabuni wengine zenye masharti nafuu.

"Tunatambua kuwa dhamana ni changamoto hivyo ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo tunahitaji mteja awe na mkataba tuu nasi tunampa mkopo wa kulipika ndani ya miezi miwili," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema mradi huo ni neema kubwa iliyoletwa na Rais na kwamba wadau wa sekta binafsi mkoani humo wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi, Angelina Ngalula, aliipongeza serikali kwa kusimamia na kuhakikisha wadau wa sekta binafsi wananufaika na miradi yote ya kimkakati inayotekelezwa nchini na si SGR.

Aidha, aliainisha vigezo vya kushiriki katika miradi hiyo kimoja kikuu ni kwamba kampuni inayotaka zabuni lazima iwe imeasisiwa hapa nchini Tanzania na yenye umiliki wa wazawa usiopungua asilimia 50.

HABARI BUNGENI

# Mbunge ataka mfuko maalum ununuzi madawati

MBUNGE wa Bunda (CCM), Boniface Getere, ameitaka serikali kujipanga kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kununua madawati ili kuondokana na tatizo sugu la upungufu wa samani hizo.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, mbunge huyo alisema ni vyema kuwapo na mfuko huo ili kuondoa tatizo hilo nchini.

"Pia nini tamko la serikali katika suala la mkanganyiko wa madawati kwenye shule za sekondari kwa kuwa kuna wanaosema madawati yanaletwa na serikali, kwingine wanasema mzazi alete dawati la mtoto wake?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema serikali imepokea ushauri huo na itaendelea kukabiliana na upungufu huo.

Hata hivyo, Silinde alisema halmashauri zinapaswa kuwa na mpango wa kutenga fedha kwa ajili ya kutatua tatizo hilo na kutumia wadau mbalimbali na kushauri wabunge kutumia fedha za mfuko wa jimbo kununua samani hizo.

Alisema serikali itaendelea kusimamia msimamo wake kwamba mwanafunzi asajiliwe kuanza kidato cha kwanza bila masharti yoyote ikiwamo ya kwenda na dawati.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji serikali inachukua hatua gani endelevu kuondokana na tatizo hilo.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawati, ili kuondokana na upungufu uliopo.

Alisema madawati 5,070,896 yameongezeka na kufanya kuongezeka kutoka madawati 3,024,311 yaliyokuwapo mwaka 2015 hadi madawati 8,095,207 Septemba, mwaka jana.

Alisema tatizo la wanafunzi kukosa madawati katika shule za msingi na sekondari limetokana na mwitikio mkubwa wa wazazi kuandikisha wanafunzi shuleni baada ya kuanzisha Mpango wa Utoaji wa Elimu Bila Malipo.

Alibainisha kuwa idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kwenye shule za msingi na sekondari umeongezeka maradufu.

"Katika kukabiliana na upungufu wa madawati, serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya utengenezaji wa madawati kwenye miradi yote inayotengewa fedha za ukamilishaji wa vyumba vya madarasa.

Pia alisema kuhamasisha wananchi na kuwashirikisha wadau na asasi mbalimbali katika utengenezaji wa madawati pamoja na kuendelea kutenga fedha ya matengenezo ya madawati kwenye halmashauri kupitia mapato ya ndani.

# Waziri asema kusoma shule binafsi si kigezo cha kukosa mkopo elimu ya juu

BUNGE limeelezwa kuwa kusoma shule binafsi za sekondari si kigezo cha mwanafunzi mwombaji kunyimwa mkopo.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo.

Katika swali lake, Tarimo alisema kumekuwa na mtazamo kuwa wanafunzi wanaosoma shule binafsi, wazazi wao wana uwezo kiuchumi, lakini ukweli ni kwamba baadhi hulipiwa ada na wafadhili au kupitia michango mbalimbali.

"Je, serikali haioni kuwa kuna sababu ya kutoa fursa sawa kuendana na ufaulu?" Alihoji.

Naibu Waziri Kipanga alisema mikopo inayotolewa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) inawalenga vijana wenye sifa za kitaaluma za kujiunga na taasisi za elimu ya juu, lakini hawana uwezo wa kumudu gharama za elimu.

"Upangaji na utoaji mikopo unaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo sura 178 ambayo inabainisha sifa za msingi za mnufaika," alisema.

Alitaja miongoni mwa sifa kuwa ni mwombaji awe Mtanzania, amedahiliwa kwenye chuo kinachotambulika, ameomba mkopo, asiwe na vyanzo vingine vinavyogharamia masomo yake.

"Aidha, kusoma shule binafsi za



Mbunge wa Viti Maalumu kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ester Bulaya, akiuliza swali la nyongeza bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




**Habari na Augusta Njoji**

sekondari si kigezo cha mwanafunzi mwombaji kunyimwa mkopo wa kugharamia elimu ya juu. Wako wanafunzi waliosoma shule binafsi na wanapata mkopo baada ya kuthibitisha uhitaji wao kwa mujibu wa vigezo vya utoaji mikopo," alisema.

Pia alisema kwa mujibu wa sheria tajwa, HESLB ina mamlaka ya kuweka utaratibu wa kubaini wahitaji.

"Kwa sababu hiyo, Bodi huandaa mwongozo unaopaswa kuzingatiwa na waombaji na kuweka masharti ya utoaji mikopo kwa mwaka husika, sifa za ziada zinazoainishwa kwa waombaji ni pamoja na uyatima, ulemavu au wazazi wenye ulemavu na wale ambao masomo yao ya sekondari au stashahada yalifadhiliwa," alisema.

# Serikali kuanzisha kituo maalum wateja

WIZARA ya Kilimo imesema iko katika hatua za mwisho kuanzisha kituo cha huduma kwa wateja ambacho mkulima atapiga simu bure alipo kutoa taarifa endapo atabaini kuna pembejeo au viuatilifu feki na ugonjwa.

Aidha, hadi sasa kuna kesi tano za wasambazaji mbolea mahakamani walikutwa wana pembejeo ambazo ni feki.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda.

Mwakagenda alisema kuna shida kubwa kwenye usambazaji wa pembejeo kwenye majimbo likiwamo Jimbo la Rungwe ambalo linalima sana viazi, lakini kumekuwapo na ucheleweshaji wa pembejeo.

"Serikali ina mpango gani kuhakikisha pembejeo zinafika kwa wakati kwa wakulima na pia wanaopewa kazi ya kusambaza pembejeo wanaleta zisizo na kiwango?" Alihoji Mwakagenda.

Bashe alisema Wizara pia inafanya ukaguzi katika maduka yote yanayouza pembejeo na pale wanapokutana na pembejeo feki, wamekuwa wakichukua hatua za kuwapeleka mahakamani wahusika.

"Ili kulitatua tatizo hili, kwa sasa biashara ya pembejeo inafanyika kwenye wilaya, lengo ni kuhakikisha mkulima anahudumiwa kwa wakati. Unaponunua pembejeo popote hakikisha umepata risiti ya kielektroniki (EFD) ya muuzaji ili tunapobaini tatizo hatua zichukuliwe," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa mwaka huu mahitaji ya mbolea nchini ni tani 700,000 na zinatakiwa ziwe zimesambazwa kuanzia Novemba, mwaka jana.

"Hadi sasa hatujapata tukio lolote la ukosefu wa pembejeo katika baadhi ya mikoa kama kuna tatizo Rungwe basi mbunge tuwasiliane tutafute ufumbuzi," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenan, alihoji mkakati wa serikali wa kuwapelekea wakulima pembejeo kwa wakati.

Akijibu swali hilo, Bashe alisema serikali huratibu mahitaji, upatikanaji, usambazaji, matumizi na kuhakiki ubora wa pembejeo za kilimo ili kufikisha kwa wakulima kwa wakati zikiwa na ubora stahiki.

Aidha, alisema serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati.

"Mikakati hiyo, ni pamoja na kupata mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo kutoka kila mkoa kabla ya msimu wa kilimo kuanza, kuwasiliana na kampuni za pembejeo na kuzihimiza kusambaza pembejeo hizo mapema kulingana na mahitaji ya kila mkoa kabla ya msimu wa kilimo," alisema.

Alisema wakulima kupitia vyama vya ushirika wanahimizwa kuainisha na kuwasilisha mahitaji ya pembejeo mapema kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ili kununua mbolea wanazohitaji kwa wakati kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja.

Alibainisha katika mwaka 2020, wakulima mkoani Iringa (kupitia IFCU) na Mbeya (kupitia MAMCOS) waliingiza mbolea moja kwa moja kutoka kiwandani Morocco (DAP) na China (UREA).

Gwiji mchumi Lipumba alipodumisha kilio chake cha miaka kisiasa, Katiba

Ukurasa 13







Ukurasa 14

**Ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje China ilivyozaa matunda**



UCHAMBUZI

# TEHAMA MPYA, UTAWALA BORA WA UTUMISHI UMMA

- Uzembe wa watawala 'stop'
- Mishahara bayana kila kona
- Mabilioni serikali yaokolewa
- Nusura ada mwaka Sh. mil. 302
- Ubunifu wa wataalamu wazawa



Aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Angellah Kairuki, alipokuwa kazini kupitia taarifa za watumishi wa umma mkoani Kagera. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mary Mwakapenda**

MAGEUZI ya kisiasa nchini kuelekea mfumo huria wa vyama vingi na kiserikali, yaliendana na kuwapo mfumo mpya wa utawala bora, hata ikaanzishwa ofisi yenye sura ya wizara ndani ya Ofisi ya Rais, ikiwa na waziri maalum.

Ni mageuzi ambayo utekelezaji wake sasa unagusa kila mahali, sehemu ya manufaiko yakishuhudiwa katika uthabiti, haki na wajibu wa utumishi na malipo ya mishahara, mishahara hewa ikibaki hadithi na kuokolewa mabilioni ya fedha za umma.

Kimsingi, usimamizi wa rasilimaliwatu katika utumishi wa umma umepitia maboresho mengi yaliyolenga kuboresha usimamizi wa watumishi na malipo ya mishahara kwa kuwezesha uwapo wa taarifa sahihi za watumishi na mishahara.

**MISHAHARA SAHIHI**

Sehemu mojawapo ya maboresho hayo, ni kumewekwa Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara Serikalini (HCMIS) ya mwaka 2010 uliounganisha Taasisi za Umma takribani 364, kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Matumizi ya Mfumo huo wa HCMIS, yaliiwezesha serikali kufanya maboresho mbalimbali, pamoja na taratibu za ajira, usimamizi wa watumishi, malipo ya watumishi, kuondoa watumishi hewa na jumla ya watumishi hewa 19,708 waliondolewa katika mfumo.

Utashi wa serikali umebeba maana kwamba, watumishi hewa hao wasingeondolewa kwa wakati, wangeingizia serikali hasara ya Sh. bilioni 19.84 (Sh. 19,838,775,680)

Aidha, ni mfumo uliofanikiwa kuwaondoa jumla ya watumishi 15,508 waliokuwa na vyeti vya elimu batili, ikiokoa wastani wa Sh. bilioni 11. 01 (Sh.11,010,680,000) zilizowalipa mshahara wa kila mwezi kwa watumishi hao.

**MABORESHO MAPYA**

Pamoja na mafanikio kupitia Mfumo wa zamani wa HCMIS, ongezeko kubwa la matumizi yake na mabadiliko ya teknolojia, yalileta changamoto katika kuusimamia, kuimarisha na kuuendeleza.

Changamoto hizo zinajumuisha kushindwa kufanya kazi kwa sehemu ya mfumo inayotoa taarifa kutoka kwa mwajiri kwenda Ofisi ya Rais Utumishi, kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Pia kuna suala la ongezeko la gharama za uendeshaji; kuongezeka watumiaji wa mfumo; wingi wa taarifa katika mfumo na ongezeko la mahitaji mbalimbali yanayochangia kuongezeka hitaji la maboresho.

Ili kukabiliana na changamoto hizo na kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu na mishahara Serikalini, mwaka 2018 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilichukua hatua za maboresho kujenga mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS).

Ni kazi ilifanywa na wataalamu wa serikali, ikijumuisha wabia: Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Mamlaka ya Serikali Mtandao na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilianza jitihada.

Lengo linatajwa ni kuleta ma-

INAENDELEA UK. 12

# TEHAMA MPYA, UTAWALA BORA WA UTUMISHI UMMA



Kaimu Ofisa TEHAMA wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Chrispinus Christian, akitoa mafunzo ya mfumo wa madeni.

INATOKA UK. 11

badiliko kutoka uliokuwa mfumo wa zamani serikalini tangu mwaka 2010 unaojulikana kama HCMIS LAWSON na sasa madhubuti wa Kitanzania, HCMIS inayoendana na mahitaji serikalini, pia mabadiliko ya teknolojia duniani.

Mfumo huo mpya, umeundwa kwa kuzingatia taratibu za utendaji kazi katika maeneo yote muhimu ya usimamizi wa rasilimaliwatu na mishahara, ukiendana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na marekebisho yake ya Mwaka 2008.

Pia kitaalamu inakidhi matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 na miongozo na nyaraka zilizotolewa kuhusiana na usimamizi wa rasilimali watu, pia mishahara katika utumishi wa umma.

Matarajio ya mfumo mpya ni kujumuisha taratibu zote muhimu za utendaji kazi, utunzaji wa taarifa muhimu za kila mtumishi wa umma, matukio yote yanayohusiana na maendeleo yake kuanzia anapoajiriwa hadi anapohitimisha utumishi.

Tofauti na ulio wa zamani, mfumo mpya wa HCMIS unajumuisha maeneo mengi yanayomhusu mtumishi na utahifadhi taarifa zake nyingi.

**MAENEO MAKUU**

Maeneo makuu yaliyojengwa katika mfumo mpya ni pamoja na taarifa zinazohusu miundo katika maeneo ya: Taasisi za umma; maendeleo ya utumishi; na mishahara yao.

Mengine yanatajwa kuwa taarifa za: Ikama (idadi ya watumishi)l bajeti; ajira; watumishi na matukio yote yanayowahusu; malipo ya mishahara, makato, marupurupu na malimbikizo yao kwa kila mwezi; upandishwaji vyeo; uhamisho; likizo; hatua za kinidhamu; upimaji wa utendaji kazi; na mahudhurio ya watumishi.

**MKURUGENZI TEHAMA**

Mkurugenzi wa TEHAMA serikalini, Priscus Kiwango, anasema maandalizi ya mfumo huo mpya yalianza kwa kukusanya mahitaji ya wadau kutoka kwenye taasisi mbalimbali za serikali, usanifu na ujenzi wa mfumo, kazi iliyoanza mwaka 2019 baada ya kukusanya mahitaji ya wadau na ulikamilika mnamo Juni jana, au miezi saba iliyopita.

Pia inalezwa kwamba kwa kutumia taarifa za ndani, serikali imeweza kuimarisha usalama wa taarifa na nyaraka za mfumo huo na kupunguza gharama za utegemezi wa makandarasi, ambayo serikali ingetumia takribani Sh. bilioni (8.5) Sh. 8,527,310,600) kama ingeegemea mfumo wa zamani.

Anasema, makadirio ni kwamba, mfumo wa awali ungegharimu

Sh. bilioni 10.31 (Sh. 10,317,881,300) kama ingenunua mfumo mbadala, sambamba na gharama hizo, serikali pia ingeendelea kulipia Sh. milioni 302 kila mwaka (Sh. 302,627,100) kwa ajili ya leseni na matengenezo.

Mkurugenzi wa Teknolojia Serikalini, anafafanua kuwa kukamilika kwa ujenzi wa mfumo huo, uliokwishafanyiwa majaribio kati ya mwezi Juni hadi Agosti mwaka jana, hivi sasa unapaswa kuanza kutumika katika taasisi zote za umma nchini.

"Kwa kuwa mfumo ni mpya, ulionekana ni vyema watumiaji wote wakapatiwa mafunzo, ili waweze kumudu matumizi yake na walengwa wakuu wa mafunzo hayo ni moafisa utumishi na maofisa tawala kutoka taasisi zote za serikali," Kiwango anasisitiza.

**WATAWALA MAFUNZONI**

Katika ufunguzi wa mafunzo ya mfumo huo kwa maofisa utumishi na maofisa tawala serikali hivi karibuni, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Francis Michael, anawataka kutumia mfumo mpya wa HCMIS kutekeleza majukumu yao.

Rai yake maalum ni kuepuka uzembe unaosababisha watumishi wa umma nchini kutolipwa mishahara yao kwa wakati, akielekeza kuwapo tatizo kutoka kwa maofisa utumishi wa baadhi ya taasisi za umma hawatekelezi majukumu yao inavyopasawa

Anakumbusha kuwa ni wajibu wao, kumtengenezea mtumishi mazingira bora kikazi ili ajisikie yuko sehemu salama na kumfanya atekeleze vyema majukumu yake kuwahudumia wananchi.

"Msiwafanye watumishi mnaowasimamia kuona sehemu ya kazi kama jehanamu. Hivyo, mbadilike kwani serikali haitomvumilia yeyote atakayekinzana na azma ya kuboresha huduma kwa wananchi," Dk. Michael anaongeza.

Katika wito huo, anawahimiza watendaji hao kitaifa kwamba wana wajibu wa kuwajengea mazingira watumishi wa umma, mambo yatakayowafanya waipende serikali katika sura ya mwitikio kwamba wanathaminiwa mchango wao kitaifa.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu Serikalini, ACP Ibrahim Mahumi, anakumbusha suala la mtumishi kukosa mshahara ni kosa kubwa na onyo lake ni kwa ofisa utumishi atakayebainika, hatua ya kwanza inahusu kusimamishiwa mshahara wake, pale mfumo mpya wa HCMIS utakapoonyesha uzembe kutoka kwake.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki mafunzoni, Mkuu wa Utawala na Utumishi, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Boniface Chatila, anaahidi kutumika mfumo mpya wa HCMIS kuleta tija katika majukumu yao na kuboresha utoaji huduma kwa umma.

Kwa mujibu wa Chatila, maeneo ya kero kuondolewa yanajumuisha watumishi wa umma kufuata huduma kutoka Ofisi ya Rais Utumishi, Dodoma, hatua walizopaswa kutekelezewa katika maeneo yao ya kazi.

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala, Wilaya ya Kondoa, Archanus Kilaja, anaipongeza serikali kuhamia mfumo mpya wa HCMISm, akitafsiri ni hatia ya kujitegemea kwenye TEHAMA.

Katika orodha ya mambo waliotakiwa kuboresha wahitimu hao maofisa utumishi na tawala hao ni usahihishaji wa taarifa za watumishi kwenye mfumo wa zamani, kabla ya kuingiza katika mfumo mpya, usioruhusu kuingiza taarifa zisizo sahihi au hazijakamilika.

Mengine ni kuongezeka uadilifu wa kiutendaji, kwa kuwezeshwa kurekodi matukio yote yatakayokuwa yakifanywa na maofisa waliopewa dhamana ya kutumia mfumo huo, hata kuimarisha uwajibikaji wao, hali inayotarajiwa kupunguza uufanyaji kazi kwa mazoea.

- ***Mwandishi wa makala hii ni Ofisa Habari Mkuu, katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.***



Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu kutoka Wilaya ya Busega, wakifuatilia mafunzo ya madeni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Gwiji mchumi Lipumba alipodumisha kilio chake cha miaka kisiasa, Katiba

## • Siku Sheria; mgeni Rais, wanasheria kibao



Prof. Ibrahim Lipumba, alipozungumza katika Siku ya Sheria nchini jijini Dodoma. Kushoto kwake ni Rais Dk. John Magufuli.

**Na Sabato Kasika**

KATIKA Sura ya Pili ndani ya katiba inayopendekezwa, inagusa Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaeleza mengi kuhusu tume hiyo, ikiwamo jinsi ya kupata viongozi wake, wajumbe na sifa zao, pia mengine mengi yanayohusu kundwa tume hiyo, ambayo vyama vya upinzani vimekuwa vikililia.

Mapendekezo ya kuwapo tume hiyo yalitolewa na wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba lililofanyika mwaka 2014 na kuingizwa kwenye Katiba pendekezi, ambayo bado haijarudishwa kwa wananchi kutoa maoni yao.

Katika hilo Mwenyekiti wa Chama cha CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, ni kati ya wanasiasa wanaoidai kwa muda mrefu, huku katika sura ya pili ndio mapendekezo kutoka kikao cha lililokuwa Bunge Maalum la Katiba.

Hata hivyo, kambi ya upinzani ilisusa kwa kutoka ndani ya vikao vya Bunge Maalum la Katiba na kuanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), kwa madai kwamba maoni ya wananchi yaliachwa, msimamo wao mkuu ni hitaji la kuwapo demokrasia.

### KUSUSISA BUNGE

Ilikuwa Aprili mwaka 2014, baadhi ya wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kutoka kambi ya upinzani, walidaiwa kuondoka kupinga walichodai kwamba maoni ya wananchi yaliyowasilishwa na Tume ya Marekebisho ya Katiba Mpya yalipuuzwa.

Walikuwa wajumbe kutoka vyama vya CUF, CHADEMA, NCCR-Mageuzi na vingine, huku wakiwa tayari wameshaanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).

Prof. Lipumba kabla ya kuondoka bungeni, alikaririwa na vyombo vya habari akilalamikia kauli alizodai hazikuwaridhisha kutoka kwa baadhi ya wajumbe, hasa walitaka muundo wa muungano wa serikali mbili.

Ni matamshi ya Prof. Lipumba, yaliungwa mkono na wajumbe wafuasi wake waliomfuata kwa safari ya kutoka bungeni muda huo. Lakini, haikuwa tamati ya kikao, kwani kiongozi wa kikao wakati huo alikiendeleza.

Hiyo ni pale alipotamka kwamba idadi ya wajumbe waliokuwapo walitosha kisheria kuendelea na kikao cha rasimu ya katiba hiyo. Jumla ya wajumbe 191 ndio waliiengua.

Ni kikao cha bunge maalum kilichokuwa na zaidi ya wajumbe 600, waliounda na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, pia wajumbe 201 wateule wa rais kutoka makundi mbalimbali ya kijamii.

### TUME HURU UCHAGUZI

Baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka jana, Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alitangaza kuwa chama chake hakitashiriki tena uchaguzi hadi tume huru ya uchaguzi iundwe.

Kwanza alisema, chama chake hakikubaliani na matokeo ya uchaguzi huo kwa madai kwamba uligubikwa na upungufu, ikiwamo hitilafu katika kuwaapisha wakala, dai likiwa limekaa kinyume cha taratibu. Mwanasiasa huyo msomi wa uchumi, aliainisha dai la kuwapo kasoro kwenye karatasi za kupiga kura, akiweka mtazamo wa mwelekeo wao ni kudai anachokifafanua kwamba haja ya kuwa na anachokiita "Katiba Mpya yenye misingi ya demokrasia na utawala bora."

Ufafanuzi wa Prof. Lipumba anaurejesha mbali kwamba, suala la ujenzi wa demokrasia linawahusu Watanzania wote.

Pia alitaja Tanzania kuwa siyo kisiwa na hata wakati wa kupigania uhuru Chama cha TANU, kilijenga uhusiano na Chama cha Labour cha Uingereza.

Hicho ni chama chenye itikadi ya mlengo wa kushoto, kama ilivyokuwa TANU na wakati huo, kama ilivyo sasa, Labour imo bungeni.

Mwanasiasa huyo anasema, katika masuala ya kudai haki kuna jumuiya za kimataifa zinazoweza kushirikishwa, lakini watakaoleta haki na demokrasia nchini wanabaki kuwa Watanzania.

### DAI LAKE JIPYA

Akiendeleza sura ileile kwenye dai la kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, anayoamini itatokea kwenye katiba mpya, mwanasiasa Prof. Lipumba, aliyekaribishwa juzi na Rais Magufuli katika 'kusalimia' kilele cha hadhira ya Wiki ya Sheria nchini, jijini Dodoma, alituma salamu zilizobeba ombi lake kikatiba akitamka:

"Nakuombea kwa dhati Mwenyezi Mungu akupe nguvu hivi viporo vyote katika kipindi hiki uweze kuvitekeleza unapomaliza kipindi chako, watu watakaoweza kulinda mafanikio ni kuwa na Katiba inayotokana na mapendekezo ya wananchi wa Tanzania."

Prof. Lipumba, pia alitanguliza imani yake ya matarajio makubwa kwamba Rais aliyeko madarakani atalifanyia kazi, hata Watanzania kushuhudia anachikitafsiri kuwa katiba itokanayo na maoni yao.

katika dokezo lake jukwaani kwenye hafla hiyo, Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mtungi, anashauri viongozi wa vyama vya siasa mwaka huu kuwa wazalendo na kuacha masuala ya kususa vikao vya bunge.

Mkasa mojawapo ni kilichotokea katika kikoa cha Bunge la Katiba, pia ilishuhudiwa mara kadhaa katika vikao vya kawaida vya Bunge la Jamhuri ya Muungano.




Hadhira katika Siku ya Sheria Tanzania, ikimsikiliza Rais Dk. John Magufuli alipowahutubia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje China ilivyozaa matunda

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibuni, Balozi wa China nchini Tanzania, Wang Ke, alifanya mahojiano na magazeti ya Habari Leo na Nipashe kuhusu ziara ya hivi karibuni ya Mjumbe wa Baraza la Taifa la China na Waziri wa Mambo ya Nje. Wang Yi, nchini Tanzania. Yafuatayo ni hahojiano kamili.

SWALI: Unaweza kutupatia muhtasari wa mambo muhimu ya ziara hii ya Mjumbe wa Baraza la Taifa la China na Waziri wa Mambo ya Nje, Wang Yi, nchini Tanzania mapema mwezi huu?

BALOZI WANG: Alialikwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania, Prof. Palamagamba Kabudi. Wang Yi alifanya ziara rasmi na ya kirafiki nchini Tanzania Januari 7 na 8.

Katika ziara yake nchini Tanzania, Wang Yi alikutana na Rais John Magufuli na alifanya mazungumzo Waziri Prof. Kabudi na baadaye walikutana na waandishi wa habari. Alihudhuria pia hafla ya utiaji saini wa mkataba wa Kubuni na Ujenzi wa Njia ya Reli ya Kiwango cha Umeme (SGR) kutoka Mwanza hadi Isaka na alizindua Kituo cha Mafunzo ya Ufundi Wilaya ya Chato. Pia alitembelea Kijiji cha Uvuvi cha Mwaloni.

SWALI: Kwa nini Wang Yi alichagua Tanzania kama kituo kimoja cha ziara yake ya kwanza nje ya nchi mwaka 2021? Kuna umuhimu gani wa ziara hii kwa maendeleo ya uhusiano kati ya China na Tanzania?

Balozi Wang: Ziara ya Waziri Wang Yi barani Afrika mwanzoni mwa mwaka imekuwa mila nzuri kwa miaka 31 na imekuwa sifa kubwa ya diplomasia ya China hasa dhidi ya kuongezeka kwa janga la COVID-19. Waziri Wang Yi amedumisha utamaduni huu na kuchukua hatua madhubuti kuonyesha umuhimu mkubwa ambao China inashikamana na Afrika na urafiki wa kindugu usiovunjika kati ya China na Afrika.

Maendeleo ya uhusiano wa kirafiki wa China na Tanzania yana nafasi muhimu katika diplomasia ya China. Uhusiano kati ya China na Tanzania una nafasi ya kuigwa na ya kuongoza katika uhusiano kati ya China na Afrika.

Machi 2013, Rais Xi Jinping alitembelea Tanzania katika ziara yake ya kwanza nje ya nchi baada ya kuchukua uongozi. Aliweka sera ya ukweli, matokeo halisi, undugu na imani nzuri. Tanzania ni mahali ambapo China ilianzisha sera yake kuelekea Afrika katika enzi mpya. Oktoba iliyopita, baada ya Rais John Magufuli kuchaguliwa tena, Rais Xi Jinping alikuwa kiongozi wa kwanza wa nchi nje ya Afrika kumtumia ujumbe wa pongezi. Desemba iliyopita, wakuu hao wawili wa nchi walifanya mazungumzo ya kihistoria kwa simu, wakichora ramani ya mwelekeo wa baadaye wa uhusiano wa nchi mbili.

Ziara ya Wang Yi nchini Tanzania katika kipindi hiki muhimu, ililenga kusaidia pande hizo mbili kujenga makubaliano zaidi, kutekeleza matokeo ya mazungumzo ya simu kati ya wakuu wa nchi na kujitahidi kupata matokeo mapema na yanayoonekana zaidi.



Ni muhimu kutajwa kuwa wakati wa ziara yake nchini Tanzania, Wang Yi alitangaza mapendekezo saba ya China juu ya kuboresha ushirikiano wa China na Afrika, ambayo yanaonyesha hadhi maalum ya Tanzania wakati wa ziara yake barani Afrika.

Ziara hiyo ilizaa matunda na ilichukua nafasi muhimu katika kukuza maendeleo endelevu na kuboresha ushirikiano kamili wa China na Tanzania. Pia ziara hii imeongeza makubaliano ya kuimarisha urafiki wa jadi kati ya China na Tanzania.

Pande zote mbili zilizungumza vizuri juu ya umuhimu wa kihistoria na wa siku hizi wa urafiki wa China na Tanzania kwa maendeleo ya nchi zote mbili na mshikamano wa China na Afrika, wakisisitiza urafiki wa China na Tanzania ni hazina ya thamani iliyoundwa na viongozi wa kizazi cha zamani wa nchi hizo mbili na inapaswa kurithiwa kutoka kizazi hadi kizazi.

Wang Yi amesema mara kadhaa katika matukio tofauti kuwa China na Tanzania ni marafiki sana ulimwenguni. Maneno yake ya kutoka moyoni na ya dhati yalijibiwa kwa uchangamfu na upande wa Tanzania.

Ziara hii imeleta msukumo katika ushirikiano wa kiutendaji kati ya China na Tanzania. Pande hizo mbili zilifanya majadiliano ya kina juu ya ushirikiano wa kufaidika katika nyanja anuwai, zilizgundua maeneo muhimu ya ushirikiano kwa hatua inayofuata na kuunda maoni mapya kwa China na Tanzania kwa pamoja kujenga Ukanda na Njia, ili kupanua zaidi masilahi yanayobadilika ya pande mbili na kuunda ukuaji mpya wa ushirikiano.

Ziara hii inatoa fursa ya kuunda ushirikiano kati ya mikakati ya maendeleo ya China na Tanzania. Nchi zote mbili zimeingia katika hatua mpya ya maendeleo na kuanza safari mpya ya kihistoria. Pande hizo mbili zilikubaliana kuwianisha vizuri Mpango wa 14 wa Miaka Mitano wa China na Ilani ya CCM ya Uchaguzi 2020-2025, kuimarisha na kupanua fursa za kimkakati zinazokabili maendeleo ya uhusiano kati ya China na Tanzania, kushughulikia vizuri shida na changamoto wakati wa ushirikiano na maendeleo, na kutoa msukumo mkubwa kwa Tanzania kufikia lengo lake la kimkakati la maendeleo huru.

SWALI: Wakati wa ziara hiyo, upande wa Tanzania umetoa maombi maalum kwa China, kama vile kuongeza bidhaa za kilimo kutoka Tanzania, kusamehe baadhi ya madeni ambayo Tanzania inadaiwa na China, na kufungua safari za moja kwa moja kati ya Tanzania na China . China itajibuje maombi haya ?

BALOZI WANG: China mara zote imekuwa ikiona umuhimu mkubwa kupanua uagizaji wa bidhaa za kilimo za Tanzania katika miaka ya hivi karibuni, na itaagiza zaidi bidhaa za ubora wa juu za Tanzania kupitia kujenga dhana mpya ya maendeleo baina ya pande mbili.

Kwanza, tutasaidia mamlaka husika wa pande zote mbili kuharakisha mazungumzo juu ya mahitaji ya ukaguzi na karantini kuhusu ufikiaji wa bidhaa za kilimo zenye ubora wa hali ya juu katika soko la China. China imefungua soko lake la tumbaku, unga wa muhogo na maharage ya soya kwa Tanzania, na itatoa fursa zaidi ya soko kwa chakula cha alizeti cha Tanzania, asali, parachichi na bidhaa zingine za kilimo.

Pili, tutatumia kikamilifu CIIE na majukwaa mengine kutambulisha bidhaa zenye ubora wa hali ya juu na rasilimali za kitalii kwa watumiaji wa China. Tatu, tutahimiza biashara nyingi za Wachina kuwekeza katika kilimo na usindikaji wa madini ya Tanzania, na kuiendeleza Tanzania kama daraja kwa kampuni za Wachina kuingia katika masoko ya mashariki na kusini mwa Afrika.

Nne, tutahimiza ushirikiano kwenye ununuaji na uuzaji wa bidhaa mtandaoni, malipo ya rununu na maeneo mengine mapya, na tufuate njia za ubunifu za kukuza biashara ya nchi mbili.

China ilizingatia umuhimu mkubwa kwa changamoto zinazosababishwa na COVID-19 kwa nchi za Afrika na inatekeleza kwa bidii Mpango wa Kusimamisha Huduma ya Deni ya G20 (DSSI). Shukrani kwa juhudi za China, G20 imeongeza kipindi cha DSSI kufikia 30, mwaka huu. Kwa sasa, China inashika nafasi ya kwanza kati ya wanachama wa G20 ambao wamefanya DSSI kwa kusimamisha dola za Kimarekani milioni 1,353 za malipo ya huduma ya deni kutoka nchi 23 pamoja na Dola za Kimarekani milioni 817 kutoka nchi 15 za Afrika.

China inazingatia suala la udhaifu wa deni la Tanzania lililosababishwa na COVID-19 kwa uzito. Pande hizo mbili zimetia saini makubaliano ya DSSI ya 2020 na kwa sasa wanajadili juu ya kusimamishwa kwa huduma ya deni ifikapo Juni 2021.

Air Tanzania kuzindua safari za moja kwa moja kati ya Tanzania na China, ambalo ni tukio kubwa katika historia ya uhusiano kati ya China na Tanzania. Itasaidia kubadilishana kwa kibinafsi, na itasaidia sana mawasiliano na uelewano kati ya nchi zetu mbili na watu wawili.

Tunatumai njia hii ya ndege inaweza kufunguliwa mapema iwezekanavyo, na kuunda mapatano thabiti ya urafiki kati ya watu wetu, na kukuza zaidi ushirikiano wa pande mbili katika nyanja kama uchumi na biashara, utamaduni na utalii katika siku zijazo.



## HABARI DODOMA

# Wanafunzi 19 wapoteza maisha matukio ya moto

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

KATIKA kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka jana, shule 44 ziliungua moto na kusababisha vifo vya wanafunzi 19, kati ya matukio 1,921 yaliyotokea, imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, Mkaguzi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Joseph Mwasabeja, alisema matukio ya kuungua moto kwa shule mwaka jana yalikuwa mengi kulinganisha na miaka mingine.

Alisema matukio hayo yamesababishwa na sababu mbalimbali na jeshi hilo linaendelea kutafuta njia ya kupunguza au kuyaondoa kabisa.

"Ajali nyingi za moto shuleni zinasababishwa na mambo mengi ikiwa ni pamoja na uzembe ambao ndio umekuwa chanzo kikubwa," alisema Mwasabeja.

Alisema pia baadhi ya sababu ni wanafunzi kutumia simu kwa siri, hivyo kuwalazimu kutoboa dari na kuchuna nyaya za umeme ili wapate sehemu ya kuchajia.

Sambamba na sababu hizo, alisema sababu nyingine ni matumizi ya pasi. Alisema wanafunzi wengi wamekuwa wakipiga pasi katika mabweni yao bila kuchukua tahadhari.

Mwasabeja alisema sababu nyingine ni migogoro kati ya uongozi wa shule na wanafunzi na wakati mwingine baina ya shule na wakazi wa maeneo ya jirani na shule husika.

"Katika shule tulizokuwa tumezichunguza na kukagua zisizozidi 21, zilizoungua kwa sababu ya hujuma ni sita, hitilafu ya umeme sita, jenereta moja, pasi mbili, gesi mbili na matukio manne hayakujulikana chanzo," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo, wamekuwa wakizishauri shule kuhakikisha zinatenga maeneo maalaum kwa ajili ya kupiga pasi pamoja na kumaliza migogoro iliyopo baina yao na wakazi wa maeneo jirani.

Pia aliitaka jamii kuhakikisha inaendelea kufuata kanuni na maelekezo yanayotolewa na serikali ili kujiepusha na majanga ya moto yanayoweza kuzuilika.

Vile vile, alitoa rai kwa wananchi, kuhakikisha ramani za majengo yao zinakaguliwa na jeshi hilo kabla ya kujengwa ili watoe ushauri ambao utasaidia pindi yanapotokea majanga mbalimbali hasa ya moto.

Mkaguzi huyo alisema kati ya matukio 1,921 ya moto yaliyotokea, katika kipindi cha mwaka jana, vifo vilikuwa 62 ikiwa wanaume 45 na wanawake 17, majeruhi 74, wanaume 52 na wanawake 22, maokozi ni 845, vifo 495 kwa wanaume 402 na wanawake 93.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma, Stella Boma (kushoto), akikabidhi msaada wa sabuni na taulo za kike kwa mzazi aliyejifungua katika Kituo cha Afya cha Chifutuka juzi, ikiwa ni wiki ya maadhimisho ya miaka 44 ya kuzaliwa kwa chama hicho. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Katibu Wazazi akemea ukataji miti

**Na Peter Mkwavila**, DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi Tanzania, Tija Magoma, amewataka Watanzania kuacha tabia ya ukataji miti ovyo hali ambayo imekuwa ikisababisha uharibifu wa mazingira.

Magoma alitoa rai hiyo juzi alipokuwa akizungumza na wazazi, walimu na wanafunzi wa Shule za Sekondari Lukundo na Itega, zilizoko kata za Nkuhungu na Changombe jijini Dodoma wakati wa upandaji miti ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sherehe za CCM kutimiza miaka 44.

Alisema suala la upandaji miti ni mpango wa Mungu, hivyo hakuna sababu ya uharibifu huo kwa kuwa wakifanya hivyo wanamkosea Mwenyezi Mungu.

"Bado kuna changamoto (tatizo) kwa baadhi ya Watanzania. Wao kazi yao ni kukata miti na kuharibu mazingira hali ambayo inapingana na serikali inayosisitiza umuhimu wa kupanda miti kila mwaka.

"Maisha ya mwanadamu kwa asilimia kubwa kila kitu anategemea miti, ukizingatia kuwa uhai kutokana na vitu vinavyopatikana kupitia miti hiyo, hivyo ni lazima ipandwe ya kutosha kuanzia kaya hadi ngazi zingine," alisema.

Kupitia maadhimisho hayo aliziomba taasisi, mashirika, vikundi mbalimbali, familia pamoja na wanafunzi, kutumia nafasi hii wakati mvua zinaendelea kunyesha kupanda miti kwa wingi.

Alisema upandaji miti kwa wakati huu mvua zinazoendelea kunyesha likitumiwa kwa umuhimu wake, linaweza kuondoa jangwa kwenye maeneo mbalimbali ambayo kuna uharibufu mkubwa wa mazingira.

Awali, Katibu wa Wazazi Wilaya ya Dodoma, Christina Masagasi, aliwataka Watanzania kupanda miti wakati wote na kuto subiri wakati wa maadhimisho kama hayo.

# Wafugaji watakiwa kwenda na wakati

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

KAIMU Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Kituo cha Mpwapwa, Aluna Chawala, amewataka wafugaji kuzingatia elimu ya ufugaji wa kisasa inayotolewa na watafiti.

Chawala aliyasema hayo jana wakati akizunguza na Nipashe kuhusiana na utafiti mbalimbali wa mifugo wanaofanya ili kuiongeza thamani na kuwainua kiuchumi wafugaji.

"Naomba wafugaji mzingatie elimu ya ufugaji kisasa inayotolewa na watafiti, mtafiti anapotoa elimu ya ufugaji mifugo anakuwa tayari ameshaifanyia kazi na kuona inafaa kwa wafugaji kuleta matokeo chanya," alisema Chawala.

Alisema wafugaji wa eneo hilo wanapaswa kuzingatia elimu inayotolewa ana watafiti katika maeneo mbalimbali wanayokwenda kutembelea.

Naye Msimamizi wa Idara ya Ng'ombe wa TALIRI Mpwapwa, Deogratius Masao, alisema utafiti mbalimbali wanaofanya kwa mifugo, una lengo la kuhakikisha jamii ya wafugaji inabadilika ikiwamo kuinuka kiuchumi.

Masao alisema wamekuwa wakiwapa elimu ya upandishaji madume na kupandikiza kwa ng'ombe wa asili ambayo wakiizingatia itawasaidia wafugaji wengi kupata mifugo bora ambayo itakakuwa ikitoa maziwa mengi pamoja na nyama endapo itachinjwa.

Pia alisema wamekuwa wakielimisha jamii ya wafugaji kuhakikisha wanatumia teknolojia hiyo ambayo itawasaidia kubadilisha ufugaji wanaofanya kadri siku zinavyokwenda.

"TALIRI Mpwapwa tunajitahidi kusambaza teknolojia hii kwa wafugaji lengo letu ni kuona kila mfugaji ananufaika na teknolojia hii, lakini kipato kinaongezeka," alisema Masao.

Alisema wafugaji wanakila sababu ya kufanya mabadiliko ya ufugaji wanaofanya hasa kipindi hiki ambacho taifa liko katika uchumi wa kati, hivyo na wao wanapaswa kubadilika ili kuendana na hali ya sasa.

Mtafiti kutoka kituo hicho, Thomas Kabuni, alisema teknolojia ya kupandikiza mimba changa kwa ng'ombe jike itasaidia wafugaji kubadili aina ya ufugaji wanaofanya.

Alisema wamefanyia utafiti teknolojia na kuonyesha kuwa haina madhara endapo itatumiwa na wafugaji itawapa manufaa na kuiwainua kiuchumi kutokana na kuwa mifugo bora yenye uhakika wa kutoa maziwa kwa wingi.

HABARI MBEYA

# Wanafunzi 89 wakaa chini kisa ukosefu wa madawati

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WANAFUNZI 89 wa Shule ya Sekondari Mwatenga, Mbarali mkoani Mbeya, wanakaa chini kutokana na ukosefu wa madawati.

Hali hiyo imemlazimu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Tamimu Lubandamo, kutoa muda wa wiki mbili watoto wote kukaa kwenye madawati.

Lubandamo alitoa maagizo hayo baada ya kujionea hali halisi ya wanafunzi wamekaa chini, huku mwalimu akiendelea kufundisha huku akiongozana na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi CCM wilaya hiyo, Abdallah Mpokwa, pamoja na Makamu Mwenyekiti.

"Nimeshangaa kuona watoto 89 wanakaa chini wakati shule hii ilianza mwaka jana, ina vidato viwili tu cha pili na kwanza nawaagiza viongozi wote wa kata hii ndani ya siku 14 waanze kukaa kwenye madawati ili wasome kwa furaha," alisema Lubandamo.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwatenga wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, wakifuatilia masomo, huku wakiwa wamekaa chini kutokana na shule hiyo kukabiliwa na uhaba wa madawati. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Odek Kipinga, alisema wanafunzi 80 wa kidato cha kwanza waliripoti kuanza masomo kati ya 100 waliochaguliwa kujiunga.

Alisema kati ya wanafunzi hao 80 watoto 67 na kufanya shule hiyo kuwa na jumla ya wanafunzi 143, huku wakiwa na jumla ya walimu sita wote wa kiume.

Vikwazo wanavyokabiliana navyo, alisema ni uhaba wa matundu ya vyoo ambapo hakuna choo cha walimu badala yake wanashea pamoja wanafunzi matundu sita.

Vilevile, aliiomba serikali kusaidia ujenzi wa nyumba za walimu kwa kuwa hadi sasa wamepanga maeneo ya mbali hutembea umbali wa kilomita 15 hadi 20 kutoka wanakoishi hadi shuleni.

Ofisa Elimu wa Kata hiyo, Anna Mmbaga, alisema hadi sasa madawati 16 yalitengenezwa na kwamba wanasubiria mengine 15 ambayo yako tayari wanatafuta usafiri kuyafuata.

Alimwahidi Mwenyekiti wa Halmashauri kuwa madawati yote yatakamilika ndani ya muda alioutoa na wanafunzi wataanza kuketi kwenye madawati.

Katika hatua nyingine Lubandamo alikanusha uvumi ulionea kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha watoto wa Shule ya Msingi Mwatenga wanakaa chini suala ambalo si kweli kwa sababu hakuna tatizo hilo na miundombinu ya mazingira yalionekana hayaendani na ya hapo.

Katibu wa CCM wa Wilaya, Abdallah Mpokwa, aliiomba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuwachukulia hatua wale wote waliohusika na upotoshaji wa video hiyo ambayo imeenea kwenye mitandao ya kijamii ikionesha watoto wa Shule ya Msingi Mwatenga wamekaa chini.

# Wazee Mbeya walilia bima za afya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ZAIDI ya wazee 500 waishio katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya wameiomba serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, kutoa bima nyingine za afya ambazo zitawasaidia kutibiwa kwenye vituo vikubwa vya kutolea huduma za afya.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkoa wa Mbeya, ambao waliwatembelea wazee hao kwa lengo la kutoa msaada na kufahamu matatizo yanayowakabili, Makamu Mwenyekiti wa Tumaini la Wazee jijini humo, Gwantwa Mwakitalima, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyolikabili kundi hilo ni kukosa bima ya afya ambayo itatumika pia kwenye hospitali.

Mwakitalima alisema kwa sasa bima walizopatiwa wazee hao zinatumika kwenye vituo vya afya na zahanati ambapo kutokana na hali zao wangepaswa kupata matibabu kwenye hospitali.

"Hitaji letu kubwa kwa sasa ni wazee hawa wasiojiweza kupatiwa bima za afya ambazo zitawasidia kutibiwa kwenye vituo vikubwa vya afya kwa sababu wanahitaji huduma bora za matibabu pamoja na vipimo kuliko ilivyo sasa ambapo wengi wao hutibiwa kwenye Kituo cha Afya cha Kiwanja Mpaka," alisema Mwakitalima.

Sambamba na hilo pia Mwakitalima aliiomba serikali na wadau wengine kuendelea kuwapatia mahitaji ya chakula, malazi na fedha kwa ajili ya matibabu wazee hao ambao wanatoka katika Kata ya Nonde, Itiji, Maendeleo na Majengo, kutokana na hali zao, hawana uwezo wa kutafuta pesa kwa ajili ya kujikimu.

Mtoa huduma ngazi ya jamii kutoka kikundi hicho cha Tumaini la Wazee, Rose Wilson, alisema moja ya vikwazo anavyokutana navyo katika kulihudumia kundi hilo ni wengi wao hawana uwezo wa kutembea kufika kwenye vituo vya kutolea huduma.

Kutokana na kikwazo hicho hulazimika kuingia gharama za kutafuta usafiri ili kuwafikisha kwenye maeneo ya kupata huduma katika kila Jumanne ya wiki.

Alisema wazee walio wengi wanakabiliwa na matatizo ya kupooza, presha na kisukari na kuwafanya wapoteze nguvu ya kujihudumia na kujitafutia riziki.

Miongoni mwa wazee waliofikiwa na Kikundi cha Wanahabari Wanawake mkoani Mbeya, Mariana Chande, alisema kutokana na uzee alionao pamoja na magonjwa yanayomsibu yamemsababishia kushindwa kufanya shughuli yoyote ambayo inamkosesha kupata hata mlo wa kila siku.

Alisema wakati mwingine hukosa kabisa hela ya kula na hana msaada wowote zaidi ya kuitegemea jamii kumsaidia.

"Hapa nilipo sina msaada wowote kutoka kwa ndugu maana karibia wote walifariki naitegemea jamii ndio initunze kwa kunipatia chakula, hela za matibabu na malazi maana nikipata hivyo naweza kujikongoja kupika," alisema Chande.

John Mbindi aliwaomba wadau wengine kuendelea kuwasaidia fedha za matibabu ikiwamo na yeye ambaye hadi sasa hawezi kutembea kwa sababu ya baadhi ya viungo vyake ambavyo ni miguu na mikono yake kupooza.

Baadhi ya waandishi wa habari akiwamo, Prakseda Mbulu, alisema licha ya kutoa baadhi ya mahitaji kwa wazee hao, lakini wanajukumu la kupaza sauti za kundi hilo ili waweze kusaidiwa.

# Waonywa kusambaza mbegu feki wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Udhibiti wa Mbegu Tanzania (TOSCI), imetahadharisha kampuni zinazouza na kusambazaji mbegu kuacha kuwauzia wakulima mbegu feki kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinawaingizia wananchi hasara.

Mkaguzi wa Mbegu kutoka TOSCI makao makuu, Dk. Mngotosha Ngomuo, alitoa tahadhari hiyo juzi, jijini Mbeya, wakati wa maofisa wa taasisi hiyo kutoka makao makuu pamoja na wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walipofanya ukaguzi wa kawaida wa mbegu kwenye maduka mbalimbali yanayouza pembejeo.

Alisema mfanyabiashara atakayekamatwa anasambaza mbegu hizo atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinafifisha juhudi za serikali kuinua kilimo.

Alizitaja mbegu ambazo zinatafsiriwa kuwa ni feki kuwa ni zile ambazo hazijakaguliwa na mamlaka hiyo na kuwekwa nembo, zilizopitwa na muda wake pamoja na zinazoingia nchini kupitia njia za panya kutoka mataifa mengine.

"Kuna mbegu imeingia nchini kinyemela ikitokea nchi jirani ya Zambia, mbegu hiyo inasemekana inapatikana mkoa wa Songwe hasa Wilaya ya Mbozi, nawaomba wananchi kuwa makini kwa kuzichunguza mbegu hizo kabla ya kwenda kupanda ili kujiridhisha," alisema Dk. Ngomuo.

Alisema kwenye ukaguzi huo walibaini kuwa mbegu nyingi zinazouzwa kwenye maduka zimepitwa na wakati na hivyo wakaziondoa ili wafanyabiashara hao wasiendelee kuzisambaza.

Kwa upande wake mkaguzi wa mbegu kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mary Kilawe, aliwataka wadau mbalimbali kushiriki kuzuia usambazaji wa mbegu hizo, akiwataka kutoiachia TOSCI peke yake.

Alisema usambazaji wa mbegu feki una madhara makubwa kwa wakulima ikiwamo kuwasababishia wakulima hasara ya kutovuna kabisa mazao kama ambavyo wanakuwa wamekusudia.

Aliwataka wauzaji wa mbegu hizo kuwa wazalendo kwa kuhakikisha wanaepuka kusambaza mbegu hizo, huku akidai kuwa wao ni wasimamizi wa sheria na hawapendi kuwachukulia hatawafanyabiashara na ndiyo maana wanatoa elimu.



# DC akerwa na mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka, amesema haridhishwi na hali ya usafi katika wilaya hiyo na kuwataka wananchi wazidishe bidii ili mazingira yawe mazuri.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Nyumba za Maendeleo Michezani ambazo zilijengwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abedi Amani Karume.

Alisema ili mji uwe safi na wa kuridhisha ni lazima mazingira yawe ya kupendeza na usafi ni wajibu wa kila mtu na si wa mtu maalum.

Rashid alisema mji ukiwa katika mazingira safi hupendeza na kuwa kivutio kwa wageni mbalimbali wanaofika nchini.

"Licha ya mji kuwa safi hupendeza pia huepukana na maradhi mbalimbali ya kuambukiza," alisema.

Pia alisema ameamua kufanya mkutano na wakazi wa nyumba hizo ili kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero zinazowakabili hasa ikizingatiwa kuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alishatoa agizo kwa viongozi aliowateua kushuka chini kwa wananchi badala ya kukaa ofisini.

Alisema serikali hivi sasa imedhamiria kuondosha matangi ya maji yaliyowekwa juu ya nyumba hizo ili nyumba hizo zibaki katika ubora wake kama zamani.

Kwa upande wao, wakazi wa nyumba hizo za maendeleo walisema wanakabiliwa na ukosefu wa huduma ya majisafi na salama na kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Waliziomba mamlaka husika kubadilisha nguzo za umeme ambazo zimechakaa na kuweka miundombinu mipya ya maji ili huduma hizo muhimu zipatikane bila usumbufu.

"Pia tunaomba hizi nyumba zifanyiwe ukarabati maana zimeshachakaa, lakini pia chemba za kuhifadhi majitaka zimeshafurika hali ambayo ni hatari kwa afya zetu," alisema Maryam Muhammed, mmoja wa wakazi hao.

# Nidhamu juu watumishi siku 100 za Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema siku 100 za uongozi wa Dk. Hussein Mwinyi, watumishi wa umma wamekuwa na nidhamu ya kazi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari wizarani kwake, Mazizini, Unguja, kuhusu siku 100 za uongozi wa Dk. Mwinyi tangu aliposhika madaraka kuiongoza Zanzibar.

Alisema hivi sasa kila mtumishi wa umma anawajibika katika utendaji wa kazi na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Alisema katika siku 100 za uongozi wa Dk. Mwinyi, watumishi wengi wamesimamishwa kazi kutokana na tuhuma mbalimbali zikiwamo za rushwa na ubadhirifu wa mali za serikali.

"Wahasibu 80 wamesimamishwa kazi kutokana na tuhuma mbalimbali za upotevu wa fedha pamoja na watumishi wengine wakiwamo wakuu wa vikosi vya ulinzi na usalama vya Zanzibar," alisema.

Watumishi hao, alisema wako katika uchunguzi kutokana na tuhuma zinazowakabili na endapo uchunguzi utakikamilika na kukutwa hawana makosa yoyote, watarejeshwa kazini na kupatiwa stahiki zao.

Alisema kikwazo kilichopo sasa ni wimbi la kesi za udhalilishaji wa kijinsia na kwamba serikali itapambana na vitendo hivyo ikiwamo kuanzisha Mahakama Maalum ya kushughulikia kesi hizo.

Haroun alisema uazishwaji wa mahakama hiyo utarahisisha ushughulikiaji wa kesi hizo ikiwamo kutoa hukumu kwa muda mrefu na kutolewa adhabu kali.

Pia alisema siku 100 za Dk. Mwinyi zimeleta mafanikio makubwa ikiwamo maridhiano ambayo yamesaidia kuondosha mivutano ya kisiasa.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Abeida Rashid (kulia), akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea magodoro 30 kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Kitwana (hayupo pichani), kwa ajili ya watoto yatima wanaoishi katika nyumba ya kulelea watoto Mazizini, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# RC atangaza kuunga mkono juhudi asasi zinazosaidia ustawi wa jamii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Mkoa Mjini Magharibi umesema utaendelea kuunga mkono sekta mbalimbali za kijamii katika kuimarisha ustawi wa jamii ndani ya mkoa huo.

Katika kufanikisha hatua hiyo, Mkuu wa Mkoa huo, Idrissa Kitwana Mustafa, alisema uongozi wa mkoa utahakikisha wadau mbalimbali wenye moyo wa kujitolea wanasaidia katika taasisi zilizomo mkoani humo.

Kitwana alisema hayo jana wakati akikabidhi magodoro 30 kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya nyumba ya kulelea watoto ya Mazizini, Unguja.

Mkuu wa Mkoa alitoa magodoro hayo kutokana na ahadi yake aliyoitoa kwa Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Sleiman Abdallah, alipofanya ziara katika nyumba hiyo na Nyumba ya Wazee, Sebleni, wiki iliyopita.

Kitwana alisema hatua ya kukabidhi magodoro hayo itapunguza baadhi ya matatizo yanayowakabili watoto katika kituo hicho na kwamba kutawapa mapumziko mazuri hatua ambayo itawejenga vyema kiafya na kiakili.

Aliutaka uongozi wa wizara kuhakikisha magodoro hayo yanatumika kwa lengo lililokusudiwa na kwamba serikali ya mkoa itafuatilia kwa karibu matumizi yake ili kuwanufaisha watoto.

Katika hatua nyingine, Kitwana aliwataka wafanyakazi wa kituo hicho kuendelea kuwapa malezi mazuri watoto wanaoishi katika kituo hicho, ili kuwajengea mustakabali mzuri wa maisha yao.

Akizungumzia elimu kwa watoto hao, mkuu wa mkoa huo, alisema wajibu wa walezi kuhakikisha wanawasimamia vizuri suala la elimu kwa watoto hao kwa kuhakikisha wanakwenda shuleni na kudurusu masomo yao wanaporudi nyumbani.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Abeida Rashid Abdallah, aliushukuru uongozi wa mkoa wa Mjini Magharibi kwa kutoa msaada huo na kuomba uongozi kuendeleza ziara za mara kwa mara katika vituo hivyo ili kubaini matatizo na kuyapatia ufumbuzi.

Kaimu Mlezi Mkuu wa Kituo cha Mazizini, Maryam Mohammed, aliiomba serikali kuendelea kukitazama kwa karibu kituo hicho hasa katika huduma za afya na elimu, huku akielezea umuhimu wa kupatiwa daktari ambaye atakuwa anaishi hapo.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAMADHANI MUSSA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1634/0341** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **SIERRA SEKONDARI** mwaka **2009.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: DAR/URA/R-B/62629/2021.**

**DAKAMWA AGROVET INPUTS LTD**
**S.L.P 400,**
**MBEYA.**
**NAMBA YA KAMPUNI : 137702940**

**YAH : TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI**

Kufuatia uamuzi wa Bodi ya wakurugenzi na wanahisa wa **DAKAMWA AGROVET INPUTS LTD** imeamua kufunga shughuli zake za biashara kuanzia tarehe **01.01.2021.**

Kwa tangazo hili watu wote ambao wanaidai **DAKAMWA AGROVET INPUTS LTD** wapeleke madai yao ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya tangazo hili katika ofisi za **DAKAMWA AGROVET INPUTS LTD** au wawasiliane kwa namba zifuatazo:

**MKURUGENZI :DAVID ANANIA KABUNGO**
**(0754-369405)**
**:CATHERINE DAVID KABUNGO**
**(0754-457833)**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AMINA NASSORO ANTONY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T 175 DKG** chasis namba **NCP600227773** engine namba **2NZ3741532** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituoc hochote cha polisi **Polisi taarifa DAR/CEN/RB/762590/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ABDALLAH SALEM MOHAMED** anatangaza kupotelewana kadi ya pikipiki ainan ya TVS yenye namba za usajili **MC 190 CES** chasisi namba **MD625AF79KIA01337** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa DAR/MAG/RB/54994/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALOYCE B MROSSO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI/CANTER** yenye namba ya usajili **T 302 AUQ** ,yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa DAR/URA/R-B/63754/2021**

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI**
**(SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB NA:CDA/ED/LA-15/………..**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: ISMAIL SEIF WA S.L.P 1249, DODOMA**
**ARDHI: KIWANJA NA.104 KITALU 'D'ENEO LA MLIMWA SOUTH**
**MUOMBAJI: ISMAIL SEIF WA S.L.P 1249 - DODOMA**

**TAARIFA IMETOLEWA**, kwamba Barua ya Toleo iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudi kutoa nakala mbadala ya barua hiyo iwapo hakuna pingamizi kwa muda wa siku thelathini (30) tokea tarehe ya Tangazo hili kutangazwa kwenye gazeti.

**BARUA YA TOLEO NAKALA HALISI** ikionekana, irudishwe kwa

**Mkurugenzi,**
**Halmashauri ya Jiji,**
**P.O.BOX 1249,**
**DODOMA.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo:** Mjini Morogoro

Usimamizi wa Mirathi Na. 30/2021.

Ombi la **SAID MOLIMO CHOROMO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ABDUL SAID MOLIMO**,

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 9/3/ 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 02/02/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODBLESS YOHANA MADADI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye namba za usajili **T 106 CNL chasisi namba SCP100369801** engine namba **ISZ0941614,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa DAR/MAG/RB/61768/2021

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Wabunge wazuiwa Myanmar, Baraza la Usalama UN lajadili

**Naypyitaw, MYANMAR**

MAMIA ya wabunge wa Bunge la Myanmar, wamefungiwa ndani ya nyumba za serikali katika mji mkuu wa nchi hiyo, huku Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, likikutana jana, kujadili mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika nchini humo.

Aidha, Marekani imetishia kuiwekea vikwazo Myanmar, baada ya mapinduzi na kumkamata Aung San Suu Kyi.

Rais wa Marekani, Joe Biden alitishia kuirejeshea Myanmar vikwazo, baada ya jeshi kupindua serikali.

Jeshi la Myanmar lilimkamata Kyi na viongozi wengine wa kisiasa, wakiwashutumu kwa udanganyifu katika uchaguzi wa hivi karibuni ambao Kyi alipata ushindi mkubwa.

Katika taarifa ya Rais Biden alisema nguvu isitumike kubadilisha maamuzi ya watu au kufuta matokeo ya uchaguzi uliofanyika kwa njia ya halali.

UN na Uingereza pia zimeshutumu mapinduzi hayo.

Marekani iliiondolea nchi hiyo vikwazo zaidi ya muongo mmoja uliopita, wakati Myanmar ilipoonyesha kufuata demokrasia.

Biden alisema hatua hiyo itapitiwa tena kwa haraka.

"Marekani itaunga mkono demokrasia kila itakapokuwa hatarini."

Katibu Mkuu wa UN, António Guterres aliitaja hatua iliyochukuliwa na jeshi kama pigo kubwa kwa mabadiliko ya kidemokrasia.

UN, imetoa wito kuachiliwa kwa watu wasiopungua 45 ambao wanazuiliwa na jeshi.

Nchini Uingereza, Waziri Mkuu, Boris Johnson ameshutumu mapinduzi hayo na kuzuiliwa kwa Aung San Suu Kyi, akisema ni kinyume na sheria.

Viongozi wa Umoja wa Ulaya (EU), walitoa shutuma zao sawa na hizo.

China, ambayo ilitoa wito wa pande zote mbili kutatua tofauti zao, huku Cambodia, Thailand na Ufilipino, zikisema kwamba hilo ni suala la ndani.

Wanajeshi walishika doria mitaani na kuwekwa amri ya kutotoka nje usiku na kutangazwa hali ya dharura kipindi cha mwaka mmoja, huku likitangaza mabadiliko katika nafasi kadhaa za mawaziri.

Kyi, kiongozi wa Chama cha National League for Democracy (NLD) na mshindi wa tuzo ya Nobel, anazuiwa na jeshi pamoja na wanasiasa wengine.

"Amiri jeshi mkuu amenyakua madaraka ya taifa ni kinyume na katiba na pia anapuuza nguvu za umma," chama hicho kilisema katika taarifa yake kwenye ukurasa wa Facebook.

Mmoja wa wabunge waliowekwa kizuizini, alisema yeye na wabunge wengine 400 hivi waliruhusiwa kuzungumza wao kwa wao wakiwa eneo hilo, ingawa walizuiwa kutumia mawasiliano ya simu za mkononi na kuondoka eneo hilo.

Mbunge huyo alisema polisi walizingira jengo hilo na askari na kulala kwa wasiwasi katika nyumba zao zilizopo eneo karibu na bunge.

"Tulilazimika kukaa macho usiku kucha," mbunge huyo aliliambia Shirika la Habari la AP, kwa sharti la kutotajwa jina lake, akihofia usalama wake.

Tangazo lililosomwa kwenye runinga ya Myawaddy inayomilikiwa na jeshi hilo, Mkuu wa Jeshi, Jenerali Min Aung Hlaing, alisema atasimamia nchi hiyo kwa mwaka mmoja.

Pia ofisi ya mkuu wa jeshi, ilitangaza majina ya mawaziri wapya 11 likijumuisha majenerali wa zamani wa jeshi, washauri wa serikali iliyopita iliyoongozwa na Jenerali Thein Sein.

***AP/DW/BBC***



Wanajeshi wa nchini Myanmar wakilinda barabara iliyowekwa vizuizi inayoelekea jengo la bunge, jana, huku mamia ya wabunge nchini humo, wakifungiwa ndani ya nyumba zao katika mji mkuu wa nchi hiyo, Naypyitaw. **PICHA/AP**

# Wakutana kujadili serikali mpito Libya

**Geneva, USWISI**

MKUTANO wa majadiliano ya kisiasa wa Libya, ulioandaliwa na Umoja wa Mataifa (UN) umefanyika Uswizi, kuamua serikali ya mpito.

Majina yatakayochaguliwa kwa serikali mpya ya mpito, yatakajumuisha wajumbe wa baraza la rais na wasimamizi wanne pamoja na Waziri Mkuu, yataamuliwa kwa kura na washiriki 75 wa Baraza la Mazungumzo ya Kisiasa la Libya ndani ya wiki moja.

Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa wa Usaidizi wa Libya (UNSMIL) Stephanie Williams, alifanya ufunguzi wa mkutano hiyo, ambayo itaendelea hadi Februari 5, mwaka huu.

Williams alibainisha kuridhishwa na idadi kubwa ya wagombea wa utawala wa serikali ya mpito ya muungano ambayo itatawala Libya hadi uchaguzi utakapofanyika Desemba 24 na kusema:

"Ninakaribisha utofauti unaowakilishwa na mrengo wa wagombea waliochaguliwa kutoka sehemu zote za kisiasa na kijamii za Libya."

Williams alisisitiza kuwa mchakato wa uchaguzi unaweza kufanywa bila kuhusisha silaha.

Pia alisema kuwa lengo ni kuwapo serikali ya mpito ya wazalendo ambao wataweza kubeba jukumu la enzi kuu ya Libya, usalama, furaha na ustawi wa watu wa Libya, badala ya masilahi ya watu wachache.

***TRT***

# Wakili adaiwa kufanya ngono kesi ikiendeshwa mahakamani

**Lima, PERU**

WAKILI Héctor Cipriano Paredes, amezua gumzo nchini Peru na duniani, baada ya kufanya ngono na mwanamke mmoja wakati kesi ikiendelea kusikilizwa kwa njia ya video mtandaoni.

Paredes, alianza kuvua nguo kisha kufuatiwa na mwanamke aliyekuwa nae na kuanza kufanya tendo hilo wakati mkutano huo ukiendelea mubashara.

Video ya tukio hilo ilisambaa kwenye mtandao wa Twitter, jana.

Tukio hilo lilikua likishuhudiwa moja kwa moja na majaji, mawakili na baadhi ya wafuatiliaji wa kesi hiyo.

Paredes alikuwa wakili wa upande wa mshtakiwa katika kesi iliyohusisha kundi la wahalifu linaloogopewa nchini humo.

Jaji John Chachua Torres, aliyekuwa akiendesha kesi hiyo, alisitisha mara moja kusikilizwa kwa kesi hiyo na kusema kuwa, Paredes ameikosea heshima mahakama.

Baada ya Jaji Torres kujiridhisha kuwa ilikuwa ni camera ya Paredes, aliamuru mara moja wakili huyo aanze kuchunguzwa na asimamishwe kushiriki katika kesi hiyo.

"Tunashuhudia kitendo cha udhalilishaji na kinaoneshwa moja kwa moja hapa, hivyo kitendo cha uchunguzi nataka wakili huyu achunguzwe mara moja," alisema Torres.

Baada ya usikilizwaji wa kesi hiyo kusitishwa, Jaji Torres aliongeza katika taarifa iliyotolewa kwa maandishi kuwa, Wakili Paredes, anatambulika kama mtu ambaye ameitia aibu mahakama, mawakili wenzake na tasnia ya sheria kwa ujumla.

Hadi sasa wakili Paredes hajatoa maelezo yoyote baada ya tukio hilo.

Mwezi Septemba, mwaka jana, mbunge mmoja, Argentina alijiuzuru baada ya kuonekana akibusu matiti ya mwanamke, wakati wa kikao cha bunge kilichofanyika kwa njia ya mtandao wa video.

BBC



# GRIEZMANN AMWITA MESSI NI GWIJI

**BARCELONA, Hispania**

FOWADI wa Barcelona, Antoine Griezmann alimtaja Lionel Messi kama "gwiji" baada ya nahodha huyo kutawala vichwa vya habari siku ya Jumapili.

Messi alianza kufunga kwa mpira wa adhabu dakika ya 20 na lilikuwa bao lake la 650 kwa Barca - kabla ya bao la Jordi Alba la kujifunga na kufanya ubao usomeke 1-1, ingawa Griezmann alifunga goli la pili na la ushindi kwa Barca dhidi ya Athletic Bilabao dakika 16 kabla ya kipenga cha mwisho.

Baada ya gazeti la El Mundo kudai mkataba ambao Messi alisaini Camp Nou mwaka 2017 - ambao unamalizika mwishoni mwa msimu - una thamani ya zaidi ya milioni 555, Griezmann aliulizwa juu ya thamani ya mtu huyo wa miaka 33.

"Tunafurahi na Messi, ni (gwiji)," Griezmann aliiambia Movistar.

"Tunatumai tunaweza kuendelea kufurahia naye na anaweza kuendelea kutusaidia kushinda."

Messi anayetajwa kuondoka Barca huku akiwa na uhusiano mzuri na Paris Saint-Germain na Manchester City, amefunga mabao mawili ya moja kwa moja kutoka kwa majaribio yake manne ya mwisho kwa Barcelona kwenye mashindano yote, baada ya kufunga moja tu kutoka kwa majaribio 62 ya awali.

Kati ya mabao 650 ya Messi kwa Barcelona, 49 kati yao yamekuwa ni ya free-kick na 38 kati ya hayo amefunga katika LaLiga.

Messi ana mabao 12 na ametoa pasi za mwisho mbili kwenye ligi hiyo kwa Barca, ambao wako nafasi ya pili na alama 10 nyuma ya viongozi Atletico Madrid.




# ASANTENI
## JUVENTUS – KHEDIRA

**BERLIN, Ujerumani**

SAMI Khedira ametuma ujumbe kwa mashabiki wa Juventus kwenye mitandao ya kijamii kuwa wakati wote atawaombea heri katika mafanikio yake.

Mshindi huyu wa Kombe la Dunia akiwa na Ujerumani 2014 alijiunga na Hertha Berlin baada ya kumaliza mkataba wake na Juventus.

"Kila safari ina mwisho. Lakini kumbukumbu zitabaki kila wakati, lilisomeka chapisho la nyota huyu mwenye umri miaka 33 kwenye ukurasa wake wa Instagram."

"Ningependa kukushukuru kwa moyo wangu wote! Ilikuwa vyema sana katika wakati wote wa mafanikio. Kama timu, tumeshinda mataji matano ya Serie A kwa miaka mitano, tukishinda Coppa mara tatu na Kombe la Super mara moja. Ninajivunia kuwa sehemu ya wakati huo."

"Kwangu imekuwa heshima daima kuvaa uzi huu wa kushinda tuzo na ninaondoka na kumbukumbu za wakati bora."

"Watu wanaifanya timu hii kuwa maalum na ninafurahi sana kuwa nimekutana na sio wachezaji wenzangu tu, bali marafiki wa kweli. Nawatakia bahati nzuri kwa siku zijazo." - Sehemu ya ujumbe wa Khedira.

Juventus pia wamechapisha katika tovuti yao ujumbe wa shukrani kwa nyota huyu. Khedira alikuwa sehemu muhimu ya Juventus licha ya ukweli kuwa hakuweza kupata nafasi ya kucheza mechi yoyote msimu huu.

# MADRID YAGOMA KUSAJILI WAPYA

**MADRID, Hispania**

DIRISHA la uhamisho la Januari limefungwa bila Real Madrid kusaini mchezaji yeyote licha ya kuruhusu wachezaji watatu kuondoka klabuni hapo kwa mkopo.

Luka Jovic alijiunga na Eintracht Frankfurt, Martin Odegaard aliondoka kwenda Arsenal na Take Kubo alihama na kujiunga na Villarreal.

Dirisha la uhamisho litafunguliwa tena majira ya joto baadaye mwaka huu, na wakati huo Madrid watakuwa wamefikisha miaka miwili bila kusaini mchezaji mpya, kwa mujibu wa Diario AS.

Usajili wa mwisho uliofanywa na Madrid ulikuwa ni wa Ferland Mendy, aliyesainiwa kutoka Lyon kwa euro milioni 48 hapo Juni, mwaka 2019.

Ilikuwa majira ya joto kwa klabu, na timu hiyo ilihitaji mabadiliko kufuatia msimu mbaya wa 2018/19 ambao klabu ilishuhudia makocha watatu tofauti wakichukua majukumu klabuni hapo.

Eden Hazard, Jovic, Eder Militao, Mendy na Rodrygo wote waliopelekwa klabuni hapo, bado hawajawa kwenye fomu nzuri sana huko Santiago Bernabeu.

Madrid walimsaini Reiner Jesus kutoka Flamengo, lakini kwa upande wa Castilla, kwa sababu za kiurasimu hawezi kuwakilisha timu ya kwanza kwa sasa kwa sababu nafasi tatu zisizo za EU zimejaa.

Real Madrid ilifunga mwaka wa fedha wa 2019/20 kwa faida ya euro milioni 313,000, na kutabiri kukadiria hasara ya euro milioni 91.1 kwa 2020/21. Pia kujumuishwa kuhusu uendeshaji wa uchumi wa klabu ni ukarabati wa Bernabeu, ambao klabu ilikopa euro milioni 575.






# UNITED
## ILIPEWA OFA KWA DZEKO

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United wanaripotiwa kupewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Roma, Edin Dzeko katika hatua za mwisho za usajili wa Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 amefunga mabao 114 katika mechi 242 kwa klabu yake hiyo ya Italia, pamoja na magoli nane katika safari 20 za mashindano yote msimu wa 2020-21.

Dzeko anaweza kuwa alicheza mchezo wake wa mwisho kwa I Giallorossi, tangu alipogombana na mkufunzi mkuu wa klabu, Paulo Fonseca.

Kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport, United walipewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji huyo kama mbadala wa Odion Ighalo, ambaye amefikia mwisho wa kipindi chake cha mkopo klabuni hapo.

Dzeko alifunga magoli 72 katika mechi 189 wakati alipokuwa na Manchester City, pamoja na mabao 50 katika safari 130 za Ligi Kuu kati ya mwaka 2011 na 2016.

United ilimsaini Edinson Cavani kwa uhamisho wa bure msimu uliopita wa kiangazi, wakati Anthony Martial, Marcus Rashford na Mason Greenwood pia wakiwa ni chaguzi za nafasi ya beki wa kati kwa mabingwa hawa wa mara 20 Ligi Kuu England.

## TAKUMI KIMEELEWEKA SOUTHAMPTON

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Southampton imefanya usajili wa mshambuliaji wa Liverpool, Takumi Minamino kwa mkopo wa mpaka mwishoni mwa msimu huu.

Watakatifu Southampton wamemsajili mchezaji huyo raia wa Japan ambaye amekosa nafasi ya kutosha ndani ya Majogoo wa Jiji la Merseyside.

Anaenda kule kuchukua nafasi ya Shane Long, ambaye ameenda kujiunga na AFC Bournemouth inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza nchini England.

Minamino mwenye umri wa miaka 26, alijiunga na Liverpool kwa ada ya pauni milioni 7.25 kutokea Red Bull Salzburg Januari ya mwaka jana.

Nyota huyo amecheza mechi nne tu tangu alivyojiunga na klabu hiyo ya Anfield.

## TUCHEL ATAKA KUBADILIKA CHELSEA

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, anataka kujifunza kutoka maisha yake ya zamani ambayo ameshuhudia akigombana na wakurugenzi wa klabu alizozifundisha.

Huko Paris Saint-Germain, Tuchel aligombana na mkurugenzi wa michezo Leonardo juu ya uhamisho katika miezi yake michache ya mwisho.

Msukosuko huo ulisababisha afukuzwe kazi mnamo Desemba mwaka jana, licha ya kushinda taji la ligi na kufikia fainali ya kwanza ya Klabu Bingwa.

Hivyo hivyo, huko Borussia Dortmund, aligombana na Mkurugenzi Mtendaji Hans-Joachim Watzke, ambaye alisema kuwa kocha huyo alimwacha akiwa "amechoka".

"Ni shauku nzuri pia ni changamoto nyingine. Neno lako ni neno lako na ninaamini neno la mtu," Tuchel aliwaambia waandishi wa habari juu ya sifa yake katika mkutano wa waandishi wa habari.

"Ninachopenda sasa na kwa nini nina maoni mazuri ni kwamba ninajitambua kuwa hili ni jambo la kuboresha, kuwa na utulivu zaidi na sio kuwa mkaidi sana katika imani yangu.

"Muundo ambao ninaona hapa ni wazi na muundo rahisi sana. Ni rahisi kuelewa kuwa hakuna watu wengi ambao hufanya maamuzi na ninaweza kuishi na hiyo.

"Wakati mambo yako wazi ni juu yangu sasa kama kocha mkuu kubadilika na kuweka maoni yangu wazi na kutoa uchambuzi wa kile ninachokiona, kile ninachohisi na ambapo pia nadhani kuwa tunaweza kuboresha na ninatumaini hii itakuja kwa njia inayofaa. "

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAJANGA YAZIDI KUIVAA LIVERPOOL

●●●Matip nje mechi zote zilizosalia za Ligi Kuu England, huku Klopp akimsifia alipambana...

**LIVERPOOL, England**

BEKI wa kati wa Liverpool, Joel Matip atakosa mechi zote zilizobakia za msimu huu kutokana na kupata majeraha ya enka.

Nyota huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Cameroon ambaye ana umri wa miaka 29 alipata majeraha hayo katika mechi iliyochezwa dhidi ya Tottenham iliyochezwa Alhamisi iliyopita na kumalizika kwa ushindi wa mabao 3-1.

Matip anaungana na Van Djik pamoja na Joe Gomez kwenye orodha ya wachezaji watakaokosekana msimu huu.

Kocha Jurgen Klopp amethibitisha kwamba, Matip atakuwa nje ya dimba kwa kipindi cha muda wote uliosalia msimu huu.

"(Matip) atakuwa tayari kurejea uwanjani wakati wa kujiandaa na msimu ujao, kila kitu kitakuwa sawa."

Licha ya kuwakosa mabeki watatu kutokana na majeruhi, Liverpool wamekamilisha usajili wa mabeki wawili ambao ni Ben Davies na Ozan Kabak wanakwenda kuziba pengo lililoachwa na mabeki hao.

Mjerumani huyo alisema Matip alipata maumivu hayo baada ya kugongana na straika wa Tottenham, Son Heung-min na ingawa alicheza mechi hiyo akiwa ni majeruhi pia.

"Ilikuwa ni bahati mbaya kwake kwa sababu alikuwa katika kuwania mpira. Alituokoa kwenye hatari kwa wakati huo katika mchezo huo dhidi ya Tottenham kwa kupambana na Son.

"Lakini aliumia enka na aliendelea na mchezo na sasa tumeambiwa atakuwa nje ya uwanja hadi msimu utakapomalizika, unaweza kuona ni namna gani alipambana kubakia uwanjani kuisaidia timu yetu," Klopp alisema.

## KWA UFUPI

**LIVERPOOL, CHELSEA VITANI**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amesema klabu mbili za Ligi Kuu England, Liverpool na Chelsea zinawania kumsajili mlinzi wa Leipzig, Dayot Upamecano mwenye miaka, 22. ***(Mirror)***

**LIVERPOOL YATOSWA**

LIVERPOOL ambayo iliwasilisha mezani ofa ya euro milioni 23 kwa ajili ya kumsajili, Duje Caleta-Car ambaye ana umri wa miaka 24, raia wa Croatia, wamekataliwa na Marseille. ***(RMC Sport, via Team Talk)***

**WILLIAMS ABANIWA**

LIVERPOOL imekataa dakika za mwisho kumwachia mlinzi wake, Neco Williams ambaye ana umri wa miaka 19 kwenda kujiunga na Southampton kwa mkopo. (***Sky Sports, via 90 Min***)

**CITY YAMKANA COSTA**

MANCHESTER City haikuwa na mpango wa kumsajili straika wa Hispania na Chelsea, Diego Costa kwa uhamisho huru licha ya kuhusishwa nae nyota huyo mwenye umri wa miaka 32. ***(Mail)***

**HAKIMI AGOMBEWA EPL**

MANCHESTER City imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Inter Milan, raia wa Morocco, Achraf Hakimi, huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 akiwa pia anatakiwa na Arsenal na Chelsea. ***(Calciomercato)***

**BARKLEY MAMBO MAGUMU**

ASTON Villa na Chelsea hazijafikia makubaliano ya kuuziana Ross Barkley mwenye umri wa miaka 27. ***(Birmingham Mail)***

**ZIDANE HALI TETE**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, lazima ashinde taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya ili kuwa na uhakika wa kazi yake. ***(AS)***

**TUCHEL AMKUBALI GILMOUR**

KIUNGO wa Scotland, Billy Gilmour mwenye umri wa miaka 19, atabakia sehemu ya kikosi cha Thomas Tuchel kwa kipindi cha pili cha msimu huu. ***(London Evening Standard)***

**CITY YAJIWEKA PAZURI**

MANCHESTER City imeongeza kujiamini katika mbio za kuwania kumsajili, Taylor Harwood-Bellis mwenye umri wa miaka 19. ***(Manchester Evening News)***

**LIVERPOOL YAMKOSA MARCELO**

LIVERPOOL imekosa nafasi ya kumsajili mlinzi wa kati wa Lyon, Marcelo baada ya klabu hiyo ya Ufaransa kukataa kumuuza nyota huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 33. ***(Sun)***

**CHUKWUEMEKA SOKONI**

KIUNGO chipukizi wa Aston Villa ambaye ana umri wa miaka 17 na ni raia wa England, Carney Chukwuemeka anafuatiliwa na Manchester United pamoja na Liverpool. ***(Times, via Birmingham Mail)***



HABARI MICHEZO

# COASTAL UNION YAIPIGIA KMC HESABU ZA KIBABE

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikitarajiwa kuendelea kesho kwa mechi za viporo, kikosi cha Coastal Union kinaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kuwavaa KMC FC katika mechi ya ligi hiyo inayotarajiwa kuchezwa ifikapo Februari 13, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema tayari ameshajiunga na kikosi hicho kwa ajili ya kurekebisha upungufu waliouona ili kuwa imara kabla ya kukutana na KMC FC.

Mgunda alisema amefurahishwa na jinsi alivyokikuta kikosi chake na hiyo inampa 'picha' kwamba watafanya kile wanachokitarajia kwenye mechi za hatua ya lala salama.

"Nimeshaungana na kikosi changu, sina wasiwasi wowote kwa sababu nilimwachia Kocha Msaidizi, Joseph Lazaro, na alikuwa akinipigia simu na kunieleza mazoezi yanavyoendelea, hata hivyo, mimi nimerudi yeye naye amekwenda kwenye timu ya vijana U-20, nami nimempokea kijiti naendelea na vijana," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema ana matumaini ya kufanya vyema kwenye raundi ya pili kwa sababu maeneo yote ambayo yalikuwa na matatizo yamejazwa na hivyo wako tayari kupambana kusaka pointi tatu muhimu katika kila mechi.

"Tumejiimarisha, kwa kifupi naweza kusema sehemu ambazo zilitakiwa kuboreshwa pia tumefanikiwa kufanya hivyo, tunajua tunakwenda kukamilisha hesabu," alisema Mgunda.

Coastal Union imesajili wachezaji sita wapya katika kipindi cha dirisha dogo ambao ni pamoja na Francis Mustapha raia wa Burundi kutoka Busarega ya Rwanda, Erick Msagati aliyejiunga kwa mkopo kutoka Polisi Tanzania na Mkongomani Paul Kitenge ambaye aliwahi kuitumikia AS Nyuki ya DRC.

Nyota wengine wapya waliotua katika klabu hiyo ya jijini Tanga ni beki wa zamani wa Yanga, Ally Ally, Jamal Dulla kutoka Namungo na mshambuliaji wa zamani mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na Kagera Sugar, Edward Christopher.

Yanga ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 44 wakifuatiwa na Simba yenye pointi 35, lakini imecheza mechi tatu pungufu wakati Ihefu FC ya Mbeya yenye pointi 13 inaburuza mkia.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (aliyekaa katikati), akiwa na makamisaa wa Ligi Kuu Bara kutoka mikoa mbalimbali baada ya kufungua semina elekezi iliyofanyika kwenye ukumbi wa hoteli ya Ngurdoto iliyoko jijini Arusha, Jumamosi iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

# Ujio wa Gomez furaha Simba

**Na Saada Akida**

BEKI wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', amesema ujio wa Kocha Mkuu mpya wa timu hiyo, Didier Gomes haujawaathiri wachezaji wa timu hiyo kisaikolojia kwa sababu wamejipanga na wako tayari kunolewa na kocha yeyote klabuni hapo.

Zimbwe aliliambia gazeti hili wachezaji wa Simba wanafahamu malengo ya timu na hivyo wamejipanga kupata matokeo chanya wakiwa na Gomes katika kila mechi iliyopo mbele yao zikiwamo za Ligi Kuu Tanzania Bara, mashindano ya Kombe la FA na hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Beki huyo alisema licha ya kuuzoea vyema mfumo aliokuwa anautumia Mbelgiji Sven Vandenbroeck, kwa sasa pia tayari wameshaanza kuingia kwenye mfumo wa Gomes na hakuna kilichowaathiri kucheza katika kiwango cha juu.

Alisema kwa muda mfupi wamebaini Gomes ni kocha mzuri na tayari wameona mabadiliko ambapo ameshatengeneza mfumo ambao una muunganiko mzuri kati ya wachezaji wapya na waliokuwapo awali ndani ya kikosi hicho.

"Sisi ni wanajeshi hatuchagui silaha, ameondoka Sven sasa amekuja Gomes, tunampa ushirikiano mzuri kuhakikisha tunafanya vyema na kufika malengo yetu ya kutwaa ubingwa wa ligi, FA na kufika mbali katika michuano ya kimataifa, ukiangalia falsafa ya kocha huyo haina tofauti kabisa na jinsi ambavyo tunavyocheza hapa Simba, nina imani tutafanya vizuri ikiwamo viporo vyetu," alisema beki huyo.

Aliongeza kikosi chao kimejipanga kushinda mechi zote za viporo na nyingine zitakazoendelea kwa ajili ya kufikia malengo yao.

"Tunakwenda Dodoma kufanya vizuri, tunafuata pointi, tutapambana kuhakikisha tunachukua pointi sita katika mechi zote mbili za viporo, hizi zitaendelea kutuimarisha kuelekea katika kampeni yetu ya kutetea ubingwa," Zimbwe Jr alisema.

## Biashara yawaita Mbao, Gwambina

**Na Saada Akida**

KATIKA kukiweka kikosi chake imara kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Biashara United ya Mjini Musoma mkoani Mara, Francis Baraza, amesema anahitaji kupata mechi mbili za kirafiki.

Baraza amezitaja mechi hizo anazohitaji ni dhidi ya 'majirani' zake Mbao FC na Gwambina FC, zote za jijini Mwanza.

Kocha huyo alisema baada ya mapumziko ya kupisha majukumu ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), kikosi kilirejea kambini na sasa anaamini ili kukaa tayari na ligi hiyo, angepata michezo hiyo ya kujipima ubavu.

"Tumefanya mazoezi kwa muda wa wiki mbili, sasa ninahitaji kucheza mechi za kirafiki, itapendeza moja ikiwa nyumbani na nyingine kutoka nje, na tukiwapata Mbao au Gwambina itakuwa kipimo kizuri kwetu," Baraza alisema.

Kocha huyo alisena ana imani mechi hizo za kirafiki akizipata zitamsaidia kuimarisha kikosi chake pmaoja na kutengeneza uelewano mzuri kwa wachezaji wapya ambao wamesajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo na wale ambao wa zamani.

## Ngorongoro kamili kuwavaa Waganda

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka cha Taifa cha vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), kinatarajia kuwakaribisha 'wababe' wao Uganda katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

Timu hizo zinatumia mechi hiyo na nyingine ya marudiano itakayochezwa Jumamosi kwa ajili ya kujiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Vijana (AFCON U-20) zitakazofanyika kuanzia Februari 14 hadi Machi 4, mwaka huu, nchini Mauritania.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Jamhuri Kihwelo 'Julio' alisema mechi hizo mbili alizopata zitakisaidia kikosi chake kujiimarisha kuelekea fainali hizo za Afrika.

Julio alisema anafahamu Uganda ina timu nzuri na itawasaidia kuwajenga wachezaji wake ambao wamedhamiria kufanya vyema katika mechi hiyo ya kirafiki.

"Niliomba kupata mechi dhidi ya Morocco, lakini imeshindikana na baada ya timu hiyo kupangwa kundi moja katika fainali zinazokuja, tumeamua kuwaomba majirani Uganda na wamekubali ombi letu la kujipima nguvu na sisi kabla ya kwenda Mauritania," alisema Julio.

# Michezo

Jumatano Februari 3, 2021

Nipashe




MAJANGA YAZIDI KUIVAA LIVERPOOL

HABARI UK 22



Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla (katikati), akimsikiliza Mshauri wa Uendeshaji wa klabu hiyo, Senzo Mazingiza (kushoto), katika hafla maalumu iliyoandaliwa kwa ajili ya mahojiano na wanahabari. Kushoto ni Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAJIPANGA KUFANYA MAKUBWA

●●●Wachezaji wake nyota, viongozi watamba msimu huu utakuwa wa...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa bado 'moto', wachezaji wa Yanga wamesema wamejiandaa kufanya 'mambo makubwa' katika msimu huu wa 2020/21 ili kuwapa furaha wanachama na mashabiki wao.

Yanga ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 44 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 35, lakini imecheza mechi tatu pungufu huku Azam FC inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 32.

Akizungumza na gazeti hili katika mahojiano maalumu yaliyofanyika kwenye kambi ya timu hiyo iliyoko Kigamboni jijini Dar es Salaam, mshambuliaji Saido Ntibazonkiza alisema kikosi hicho kimejiandaa kusaka matokeo mazuri katika kila mechi watakayocheza.

Ntibazonkiza alisema wanafahamu ushindani uliopo kwenye ligi hiyo ni mkubwa, lakini wanaamini watatimiza malengo yao kwa sababu wamejiandaa vizuri na wana kikosi chenye uzoefu wa kufikia malengo yao.

Nyota huyo ambaye anaichezea Timu ya Taifa ya Burundi alisema kila mchezaji wa Yanga anafahamu malengo ya klabu yao na kwa sababu hiyo, kwao kila mechi watakayocheza itakuwa ni sawa na fainali.

Aliongeza ili kufikia mafanikio yao, wanaomba wanachama na mashabiki waendelee kuwaunga mkono katika kipindi hiki cha kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano yote watakayoshiriki.

"Tumejipanga kuhakikisha malengo yetu yanatimia, tutafanya mambo mazuri, tuna kikosi imara na kila mmoja anawaza ubingwa, Kikombe cha Mapinduzi kimetuongezea hamasa ya kuendelea kupambana ili kushinda mataji mengine, tunatarajia kuwa na msimu wenye mafanikio," alisema Ntibazonkiza.

Kuhusu ujio wa Fiston Abdulrazack, Ntibazonkiza alisema anafahamu uwezo wa nyota huyo mpya na anaamini atakuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha Yanga inafanya vizuri katika msimu huu utakaoendelea kuanzia Februari 13, mwaka huu.

Alisema Fiston ni mmoja wa wachezaji mahiri kwenye ukanda huu na endapo atakuwa na afya imara, ataiongezea nguvu Yanga kama ilivyotarajia wakati inamsajili.

"Mimi huwa sipendi kutoa ahadi, kwa sababu sijui huko mbele kuna nini na kuhusu Fiston, Yanga watarajie makubwa kama afanya yake itakuwa nzuri, kama kila kitu kitakwenda sawa, ninaamini atafanya makubwa pia," aliongeza.

Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, alisema anawashukuru wadhamini na wafadhili mbalimbali wanaoisaidia klabu yao kufikia malengo waliyojiwekea katika kipindi hiki chenye ushindani.

"Tunajivunia kuona timu zetu zote mbili, Yanga na Yanga Princess ambazo kwa sasa ndiyo zinazoongoza katika ligi zinazoshiriki, pia tunawashukuru wadhamini wakuu wa klabu yetu, SportPesa pamoja na wafadhili wetu GSM kwa kuendelea kuiopa sapoti Klabu ya Yanga na pia tunawaomba waendelee kutushika ili tuweze kufikia malengo tuliyoweka," alisema Msolla.

Naye Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, Hersi Saidi, alisema kampuni yao inafurahishwa na kuridhishwa na utendaji kazi unaofanywa na viongozi Yanga na wanaahidi wataendelea kushirikiana nao.

"Tunawaomba mashabiki na wapenzi wa Yanga kuendelea kuisapoti na kuipambania klabu, tunaahidi kama GSM tutaendelea kuisapoti kwa asilimia 100," alisema Hersi.

## SIMBA YAFUATA BARAKA BUNGENI

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wamesema wako tayari kusaka pointi tatu muhimu katika mechi ya 'kiporo' dhidi ya Dodoma FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, ili kuendeleza kampeni yao ya kuwania taji la ligi hiyo wanalolishikilia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kikosi chao kinakwenda Dodoma kwa kazi moja ya kufuata pointi tatu ili wajiimarishe kwenye mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo.

Manara alisema mazoezi waliyopata katika mechi za mashindano ya Simba Super Cup yatawasaidia kuondoka na matokeo chanya na baadaye kurejea jijini kuwasubiri Azam FC katika mchezo mwingine utakaochezwa Februari 7, mwaka huu.

"Kikosi kinaanza maandalizi kwa ajili ya ligi, tutaondoka asubuhi Jumatano ili kwenda Dodoma kwa ajili ya mchezo wetu wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Dodoma Jiji FC ambao utachezwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma, lakini tutapata nafasi ya kwenda bungeni Februari 3, mwaka huu.

"Bungeni tutakwenda kupata baraka za wabunge wetu hasa ukizingatia kwamba tunakwenda kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika. Februari 5 baada ya mchezo wetu tutarudi Dar es Salaam kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wetu dhidi ya Azam FC," alisema Manara.

Aliongeza wanafahamu Dodoma FC ni moja ya timu zenye ushindani katika Ligi Kuu Bara wanapokuwa nyumbani, lakini wao wanaenda Dodoma kuchukua pointi muhimu ili wafikie malengo yao kama walivyokubaliana wakati wanaanza msimu huu.

Baada ya mechi hiyo ya kesho, Simba inayonolewa na Mfaransa Didier Gomes ambaye alichukua mikoba ya Sven Vandenbroeck itarudi jijini kuwasubiri Azam FC katika mchezo mwingine wa kiporo utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002